**MBARONI** tuhuma kuchinja msichana mwenye ulemavu

UKURASA 9

**NHIF** yaridhia Hospitali Aga Khan kusitisha huduma kwa wanachama

UK. 3



**RAIS** Samia kukabidhiwa skuli ya kisasa na Benki NMB

UKURASA 17


Nipashe Spotika

MAWINGA WATANO WANAOIFAA BARCA KAMA IKIMKOSA WILLIAMS

ISIKUPITE

UKURASA 11


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumatatu Agosti 12, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581766

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# CHADEMA, polisi wapimana ubavu

**MSAJILI** aingilia kati, Lissu ajitosa na swali kwa jeshi...*ukurasa 2*



John Mnyika

Kamishna wa Polisi Awadh Juma



Rais Samia Suluhu Hassan akipokewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Rwanda, Judith Uwizeye, baada ya kuwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Kigali kuhudhuria sherehe za uapisho wa Rais Mteule wa Rwanda, Paul Kagame. **PICHA: IKULU**

# 'Mchawi' mpya aibuka baa la ajali barabarani

UKURASA 3

## Wabuni mchele joto unaoondoa tatizo la kitambi, shinikizo la damu

UKURASA 7

**MICHEZO** **SIMBA WAWATULIZA MASHABIKI** UK 24

**MAONI, KATUNI UK.6**

# CHADEMA, polisi wapimana ubavu

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimetunishia msuli Jeshi la Polisi na Msajili wa Vyama vya Siasa, kikisisitiza kitafanya kongamano la maadhimisho ya Siku ya Vijana licha ya kuwapo zuio.

Chama hicho kimepanga kufanya maandamano ya amani mkoani Mbeya na kufanya mkutano katika Uwanja wa Ruanda Nzovwe, jijini Mbeya, ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani.

Hata hivyo, taarifa iliyotolewa jana na Jeshi la Polisi nchini kupitia kwa Kamishna wa Operesheni na Mafunzo, Kamishna wa Polisi Awadh Haji na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, zilipiga marufuku mkutano wa chama hicho.

Akizungumza na Nipashe jana, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema pamoja na makatazo hayo, wataendelea na shughuli yao kama walivyopanga na hawako tayari kuahirisha kongamano hilo ambalo wamefanya maandalizi kwa muda mrefu.

"Katazo la Msajili na Jeshi la Polisi ni ukiukwaji wa sheria za nchi. Kwa hiyo, sisi tunaendelea na maandalizi na kesho (leo) tutaendelea na maadhimisho yetu ya Siku ya Vijana Duniani kama ambavyo tumepanga," alisema Mnyika.

**"Katazo la Msajili na Jeshi la Polisi ni ukiukwaji wa sheria za nchi. Kwa hiyo, sisi tunaendelea na maandalizi na kesho (leo) tutaendelea na maadhimisho yetu ya Siku ya Vijana Duniani kama ambavyo tumepanga," alisema**

Katibu Mwenezi wa Umoja wa Vijana wa Chama hicho (BAVICHA), Twaha Mwaipaya, alisema wanaendelea na maandalizi na watahakikisha maadhimisho hayo yatafanyika kwa mafanikio kama ambavyo wamepanga.

Alisema kauli zilizonukuliwa na Jeshi la Polisi ni za kwake na kwamba kauli hazina ukomo na hivyo haziwezi kusababisha kongamano kuahirishwa.

"Kama nilifanya makosa kutoa kauli hizo zilizonukuliwa na Jeshi la Polisi na Msajili wa Vyama vya Siasa, basi wangenishikilia mimi lakini si kutumia mwanya huo kuzuia kongamano, kama litaahirishwa basi tutakuwa tumeahirisha sisi lakini si kauli hizo," alisema Twaha.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Mbeya jana, Kamishna wa Operesheni na Mafunzo wa Jeshi la Polisi, CP Awadh Haji alisema jeshi hilo liliamua kupiga marufuku mkutano huo kutokana na matamko yanayotolewa na viongozi wa chama hicho kuashiria uvunjifu wa amani.

Alisema mbali na kupiga marufuku maandamano hayo, pia limezuia mikutano na mikusanyiko ya ndani na nje ya vijana wa chama hicho na kwamba wakikaidi amri hiyo, watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

Alisema baadhi ya matamko ya viongozi wa vijana wa CHADEMA yanaashiria



Tundu Lissu

kuwa wanataka kufanya vurugu kama ambavyo ilitokea hivi karibuni Kenya ambako vijana walifanya maandamano na fujo katika maeneo mbalimbali.

Alisema kauli zilizotolewa na Katibu Mwenezi wa BAVICHA, Mwaipaya, ziliashiria kuhamasisha vijana kufanya fujo na ndio maana waliamua kuzuia.

"Moja kati ya kauli zilizotolewa na Mwaipaya ni 'kama kijana yeyote unaipenda nchi yako ya Tanzania, umeshalia miaka yako yote, siku ya tarehe 12/08/2024 tunakwenda kuweka hatima ya taifa letu la Tanzania mkoani Mbeya, kwa hiyo kijana yeyote popote Tanzania, njoo Uwanja wa Ruanda Nzovwe Mbeya'. Kauli hizi zinaashiria nia ovu," alisema Kamishna Haji.

Kauli nyingine ambazo zinadaiwa kutolewa na Mwaipaya alinukuu CP Awadh kuwa "Tupo serious sana na jambo hili, kwa hiyo vijana wote CHADEMA kama ambavyo vijana wa Kenya wamejitambua, siku ya tarehe 12/08/2024 tunakwenda kuacha uteja kwa serikali, vijana wa kitanzania na kuweka maazimio makubwa ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu mwaka 2025'.

Kamishna huyo alisema jeshi hilo linashauri vijana wa CHADEMA wa mikoa mbalimbali wanaopanga kwenda mkoani Mbeya kushiriki maadhimisho hayo kuahirisha ili kuepuka alichokiita "kushughulikiwa".

"Kufuatia kauli hizo na matamko mbalimbali yanayotolewa na viongozi hao, Jeshi la Polisi limeamua kupiga marufuku maandamano na mikusanyiko ya aina yoyote ile ya ndani au nje inayotaka kufanyika kwa mwamvuli wa kuadhimisha Siku ya Vijana Duniani, inalenga kuleta uvunjifu wa amani Mkoa wa Mbeya na maeneo mengine yoyote katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Hivyo basi, Jeshi la Polisi nchini linatoa onyo kali na katazo kwa mtu au kikundi cha watu kinachojipanga kufanya maandamano na mikusanyiko, kuacha mara moja kwani Jeshi la Polisi lipo imara na limejipanga vizuri kuhakikisha ulinzi, usalama, amani na utulivu vinatawala nchini na lipo tayari kuzuia na kupambana na viashiria vyovyote vya uvunjifu wa amani, na halitasita kuchukua hatua kali kwa mujibu wa sheria kwa mtu yeyote atakayekiuka katazo hili," alisema CP Awadhi katika taarifa yake hiyo.

**IRINGA**

Mkoani Iringa jana, zaidi ya viijana 150 wa CHADEMA walizuiwa na kuwekwa kizuizini kwa saa kadhaa katika Kituo Kikuu cha Polisi mjini Iringa wakiwa njiani kwenda jijini Mbeya kwa ajili ya kushiriki kongamano la vijana lililoambatana na maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani.

Vijana hao wa BAVICHA kutoka Kanda ya Kaskazini katika mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro walizuiwa baada ya kuwasili mkoani Iringa eneo la Kihesa, Kilolo, Manispaa ya Iringa kwa kile kinachodaiwa ni maelekezo kutoka juu yaliyolitaka jeshi hilo kuzuia safari ya vijana hao baada ya kubaini kuwapo hali ya hatarishi kwa usalama wa raia.

Baadhi ya viongozi wa vijana hao, akiwamo Emma Kimambo, walidai wako safarini kwenda mkoani Mbeya kwa ajili ya maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani, lakini walizuiwa kwa madai ya kufanyiwa mahojiano na Jeshi la Polisi na kutakiwa kwenda kituo cha polisi.

"Sisi tupo safarini kuelekea jijini Mbeya kama vijana wa CHADEMA, sisi siyo wahalifu, bali ni vijana wazalendo tunaelekea kwenye maadhimisho ya Siku ya Vijana Duniani, lakini tumefika Iringa tumezuiwa na Jeshi la Polisi, hatukatai kama kuna changamoto tuambiwe sheria ichukue mkondo wake, tumejaribu kuuliza tumeambiwa ni maelekezo kutoka juu tunatakiwa kwenda kituo cha polisi kuhojiwa," alisema Kimambo.

Nipashe ilimtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, SACP Allan Bukumbi kutaka kupata taarifa zaidi kuhusu suala hilo bila mafanikio baada ya simu yake kutopatikana.

**LISSU, MSAJILI**

Katika ukurasa wake wa X, Makamu Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Tundu Lissu alisema kinachofanyika kuzuia kongamano hilo si sawa kwa kuwa Siku ya Vijana Duniani inasherehekewa duniani kote, akihoji sababu za polisi kuweka zuio.

Jana Naibu Msajili wa Vyama vya Siasa Tanzania, Sisty Nyahoza, aliwataka viongozi wa CHADEMA kusitisha kongamano hilo.

Barua ya Msajili kwenda kwa Katibu Mkuu wa CHADEMA, Mnyika, inaeleza kuwa kauli zilizotolewa na Katibu Mwenezi wa BAVICHA, Mwaipaya ni ukiukwaji wa Sheria ya Vyama vya Siasa.

"Msajili anawaasa viongozi wa CHADEMA kusitisha shughuli yoyote mliyopanga kufanya siku ya Agosti 12, 2024 Mbeya au mahali popote nchini, ambayo mnajua itasababisha uvunjifu wa sheria, amani na utulivu.

"Maelezo ya Katibu Mwenezi wa BAVICHA katika video hiyo yanakiuka Sheria ya Vyama vya Siasa na yanaashiria mkusanyiko huo unaweza kutumika kuhamasisha vijana kufanya vitendo vya uvunjifu wa sheria kama ilivyotokea Kenya," alisema.

Msajili pia ameelekeza Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, Katibu Mkuu wake, Mnyika na Mwenyekiti wa BAVICHA, John Pambalu kufika Ofisi ya Msajili, jijini Dar es Salaam kesho Agosti 13,2024 saa 5:00 asubuhi kueleza kuhusu suala hilo.

***Imeandikwa na Nebart Msokwa (MBEYA) na Agustino Kihombo (IRINGA)**


Tanzania Human Rights Defenders Coalition
[THRDC]

P. O. Box 105926 Dar es Salaam, Tanzania
Mob: +255 769 642 208 E-mail; info@thrdc.or.tz
Website: www.thrdc.or.tz

**KUMB: THRDC/AGM/Vol.1/2024**

**NOTISI YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TATU WA WANACHAMA (THRDC)**

Kwa wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa Wanachama wa Mtandao 2024.

**HII NI TAARIFA RASMI KWAMBA;** Mkutano Mkuu wa Kumi na Tatu (13) wa Wanachama wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) utafanyika wa **siku ya Jumatano tarehe 11 mwezi Septemba** kuanzia saa kumi alasiri mpaka saa kumi na mbili jioni katika ukumbi wa **Mt. Meru Hotel jijini Arusha** na **kwa njia ya Mtandao.**

Ajenda zifuatazo zitajadiliwa:

13.1) Kuhakiki Akidi ya Mkutano Mkuu waliohudhuria.
13.2) Kufungua Mkutano.
13.3) Kuthibitisha na Kupitisha Ajenda.
13.4) Kuidhinisha Kumbukumbu za Mkutano Uliopita wa mwaka 2023
13.5) Yatokanayo na Mkutano uliopita.
13.6) Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi ya 2023.
13.7) Taarifa ya fedha iliyokaguliwa ya mwaka 2023.
13.8) Taarifa ya mpango kazi mwaka 2024.
13.9) Hali ya Uanachama;
  i. Kufuta wanachama wanaodaiwa miaka miwili kwa mujibu wa katiba ya Mtandao.
  ii. Kuaga waratibu wa kanda ya pwani ya mashariki, na kanda ya magharibi, na kanda ya ziwa mashariki.
  iii. Kukaribisha waratibu wa kanda wapya.
13.10) Kuaga mjumbe wa bodi aliyestaafu .
13.11) Kuwatambulisha wanachama wapya wa Mtandao.
13.12) Taarifa kuhusu utekelezaji wa mkakati wa uendelevu wa Mtandao.
13.13) Kufunga Mkutano.

**NOTISI HII IMETOLEWA RASMI LEO HII TAREHE 12/08/2024.** Tunategemea kupata maoni yenu kuhusu ajenda zilizopendekezwa kabla ya tarehe **01/09/2024.**
Sajili ushiriki wako kupitia barua pepe **membersaffairs@thrdc.or.tz** kabla ya tarehe **1 Septemba 2024.**

**Ikumbukwe kwamba, Wanachama waliokamilisha vigezo vya uanachama kama inavyoeleza Katiba ndio watakaokuwa na haki ya kuhudhuria mkutano huu. Inasisitizwa kwamba, gharama za ushiriki wa mkutano huu zitagharamiwa na mwanachama mwenyewe kwa mujibu wa katiba ya Mtandao.**

**Onesmo Olengurumwa, Adv**

**Mratibu Kitaifa**
**Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC)**

# NHIF yaridhia Hospitali Aga Khan kusitisha huduma kwa wanachama

**Na Mwandishi Wetu**

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umeridhia ombi la Hospitali ya Aga Khan kusitisha huduma za matibabu kwa wanachama wa mfuko huo kuanzia kesho kutokana na sababu za kiuendeshaji.

Taarifa ya NHIF iliyotolewa jana na Grace Michael, Kaimu Meneja Uhusiano wa mfuko huo, ilibainisha kuwa kwa mujibu wa mkataba wa mfuko na mtoahuduma, upande wowote unayo haki ya kuomba kusitisha au kuendelea na utoaji huduma.

"Hivyo, Aga Khan kama ilivyo kwa vituo vingine, anao uhuru wa kutumia haki ya kimkataba. Wakati majadiliano na mtoahuduma yakiendelea kuhusu maombi yake ya kusitisha huduma, mfuko unatoa taarifa kwa wadau wake kuwa ifikapo tarehe tajwa hapo juu, wanachama wanashauriwa kutumia vituo mbadala vilivyosajiliwa na mfuko kupata huduma za matibabu.

"Mfuko umesajili zaidi ya vituo 9,000 ambavyo vinamilikiwa na serikali, taasisi binafsi na mashirika ya dini. Vituo hivyo ni vya ngazi mbalimbali kuanzia zahanati hadi ngazi ya Hospitali ya Taifa ya Rufani.

"Lengo la kusajili vituo hivyo ni kumpa uhuru mwanachama kuchagua kituo cha kupata huduma za matibabu popote alipo ndani ya nchi," alisema Grace katika taarifa yake hiyo.

Aliongeza kuwa mfuko umefanya maandalizi ya kuwezesha mwendelezo wa huduma kwa wanachama waliokuwa wanapata huduma katika Hospitali ya Aga Khan ikiwamo kusajili vituo mbadala vyenye hadhi sawa au zaidi ya hospitali hiyo.

"Ofisi za NHIF nchini pamoja na Kituo cha Mfuko cha Huduma kwa Wateja zimejipanga kuhakikisha wanachama hawakosi huduma katika kipindi cha mpito.

"Hivyo, endapo mwanachama atapata changamoto yoyote, awasiliane na mfuko kupitia ofisi zake zilizoko nchi nzima pamoja na Kituo cha Huduma kwa Wateja kinachofanya kazi saa 24 kila siku kupitia namba 199 bila malipo," alisema Grace.



Mhamasishaji wa ujenzi wa daraja katika eneo la Kwa Nipe Malamba Mawili, Dar es Salaam, Jonas Kilamla (kulia), akielezea jinsi yeye na wakazi wenzake walivyochangishana fedha kwa ajili ya ujenzi huo walipokuwa wakichimba msingi jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# LATRA: Uchovu chanzo ajali madereva mikoani

**Na Christina Mwakangale**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imesema tangu kuanzishwa Mfumo wa Ufuatiliaji Gari (VTS-Vertical Tracking System) umedhibiti ajali zitokanazo na mwendokasi, lakini hivi sasa kuna matukio ya ajali yatokanayo na uchovu wa madereva.

Uchunguzi uliofanywa na LATRA unaonesha kwa kipindi cha Julai mwaka huu katika ajali 15 zilizotokea, nane zilitokea alfajiri na zilisababishwa na uchovu wa madereva.

Bingwa Mbobezi wa Mfumo wa Fahamu (Neurologist) kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila, Dk. Henrika Kimambo, anasema kuendesha gari na uchovu ni sawa na kuendesha ukiwa umelewa.

Bingwa Mwandamizi wa Afya na Magonjwa ya Akili kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Saidi Kuganda, amesema uchovu huathiri akili na humsababishia anayeendesha chombo cha moto au mashine kukosa umakini.

Akifafanua kuhusu ajali za barabarani na mifumo mbalimbali, Ofisa Mdhibiti Ubora (Quality Assurance Officer) kutoka LATRA, Japhet Kabelege, alisema mamlaka hiyo sasa inakuja na mbinu mpya ya kufuatilia mwenendo wa dereva akiwa safarini, asiendeshe gari zaidi ya saa nane, kama ilivyo kisheria.

Kabelege aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati LATRA ilipotoa mafunzo kuhusu kanuni mpya za udhibiti wa usafiri wa nchi kavu, kwa waandishi wa habari kutoka Taasisi ya Waandishi wa Habari za Usalama Barabarani (TRSJNET) pamoja na Taasisi ya Waandishi wa Habari za Afya ya Akili (TAMHJO).

"LATRA imeimarisha matumizi ya teknolojia kwa kutumia mifumo ya kidigitali katika ukusanyaji wa taarifa na mienendo ya madereva pindi wanapokuwa barabarani, kuimarisha usalama barabarani. VTS imeanzishwa mwaka 2017 na matokeo ni chanya.

"Tunatarajia kuja na mfumo wa kamera ambao utaanza kufuatilia basi yaani idadi ya abiria hasa wanaozidi kwenye gari na yanayoendelea ndani ya gari. Kamera itapima uchovu, ujazaji wa abiria na mwenendo.

"Baadaye mabasi yote yatakuwa na kamera zipatazo tatu pande tofauti za basi, mbele, nyuma na alipo dereva.

"Hadi Julai 31 idadi ya magari yaliyosajiliwa katika mfumo wa VTS ikiwamo ya kukodiwa binafsi (special hire), mabasi ya wanafunzi na ya abiria 10,850. Kusajili gari katika mfumo huu ni lazima, ili kufuatilia gari hasa ya abiria.

"Mfumo huu husaidia kutoa taarifa kutoka kwetu kwenda kwa mkoa husika na iwapo basi linatembea kwa mwendokasi hatua zitachukuliwa mara moja.

"Ajali za Julai mwaka huu, nyingi zilizotokea hazikuzidi mwendokasi ulikuwa 77 na 83 au 67 kabla ya ajali. Asilimia kubwa sio ajali za sababu ya mwendokasi, ila uchovu na uzembe wa madereva ndio sababu kuu.

"Tulibaini basi lililotumbukia mtoni, tulipomfuatilia dereva tulibaini aliendesha zaidi ya saa 12 na abiria mmoja aliyehojiwa alisema dereva alisinzia na aliungamisha safari ndefu akielekea pia Tunduma.

"Tunakuja na mfumo wa 'i-button' na itakuwa takwa la lazima na kisheria mmiliki wa basi afunge mfumo huu, pamoja na VTS utakaofuatilia mwenendo wa dereva na basi lote.

"Mfumo huu utamfuatilia dereva na kumsoma dereva na baada ya saa nane italeta taarifa namna anavyoendesha akizidisha muda huo, tutajua na atakuwa amevunja sheria," alisema Kabelege.

"Hadi Julai mwaka huu, magari 2,488 yalikuwa yamesajiliwa katika mfumo wa 'i-button'."

Ofisa Leseni na Usajili LATRA, Mbwana Ndaro, alisema ajali inapotokea mfumo wa VTS unaonyesha mwendokasi na eneo ilipotokea.

**"Tunatarajia kuja na mfumo wa kamera ambao utaanza kufuatilia basi yaani idadi ya abiria hasa wanaozidi kwenye gari na yanayoendelea ndani ya gari. Kamera itapima uchovu, ujazaji wa abiria na mwenendo.**

"Mfumo huu umesaidia ingawa wapo wachache ambao wanachezea mfumo wa VTS. Madereva 24 wamesitishiwa leseni kwa mwendokasi Julai, mwaka huu."

**ATHARI ZA UCHOVU**

Dk. Kuganda amesema kufanya kazi bila kupumzika kuna athari. "Ukifanya kazi nyingi kupita uwezo wako na kwa muda mrefu utachoka mwili na akili. Kitakachofuata ni 'burn out'...mwili umechoka na akili pia imechoka. Hii ni dalili ya kisaikolojia.

"Lakini kwa mtu ambaye hapumziki, anaona hana haja ya likizo ni mfanyakazi bora au dereva anaendesha muda mrefu hii inaweza kusababisha kuondoa umakini na kukosea kile anachokifanya kama ajali au kuharibu kazi.

"Pia anaweza kupoteza usingizi ukienda hospitali kwa daktari mzuri atakwambia ukapumzike. Na ndio maana katika utumishi wa umma, ni lazima likizo ukapumzike, ile ina maana kiafya sio ilizuka tu."

Bingwa Bobezi wa Mfumo wa Fahamu (Neurologist) kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH)-Mloganzila, Dk. Kimambo, anasema, "Mojawapo ya kazi ya ubongo ni kufanya uamuzi, kuwa makini, ufanisi, kumbukumbu. Kuwa na mwitikio wa haraka kutokana na vichocheo vilivyomo kwenye mazingira husika.

"Uchovu (fatigue) husababisha kiwango cha juu cha inflammation mwilini na mabadiliko ya homoni (ambazo huhusika katika nguvu na kuzingatia jambo).

"Hivyo basi 'fatigue' huathiri utendaji kazi wa ubongo na kusababisha kupungua kwa umaskini, kutofanya maamuzi sahihi kwa wakati, kuchelewa kwa mwitikio wa mwili kwa vichocheo vya nje/mazingira," alisema bingwa huyo.

Alisema mfumo wa kumbukumbu kutofanya kazi kwa ufanisi huchangia au husababisha ajali kutokea na utafiti unaonesha, kuendesha gari ukiwa mchovu ni sawa sawa na kuendesha gari ukiwa umelewa.


hosplan

**Job Opportunity: Key Client Relation**

**Location:** Dar Es Salaam | Position: **Full-Time**

We are a leading global healthcare services company looking for a dynamic, energetic, and well-mannered Health Executive to engage with high-end clientele and guide them through accessing advanced medical treatments across the world.

**Key Qualifications:**

- Minimum graduation; healthcare background preferred.
- Good schooling and educational background.
- Strong communication and interpersonal skills.
- Ability to engage with high-end society and provide personalized support.

**Benefits:**

- Competitive compensation.
- Opportunity to work with a prestigious clientele.
- Professional development and growth opportunities.

**How to Apply:** Submit your resume to **amit@hosplan.com / WhatsApp:- +255748555889**

Application Deadline: **16th August 2024**

***Join us and make a difference in healthcare—apply today!***



**KATIKA BARAZA LA MIRATHI NA NYUMBA**

**WILAYA YA KINONDONI MWANANYAMALA**

**SHAURI LA MADAI NAMBARI 120 LA 2024**

**TACH BOARD LTD ......MUOMBAJI/WAOMBAJI**

**DHIDI YA**

**SWALLOW INVESTMENT (T) CO. LTD...MDAIWA/WADAIWA**

**WITO KUITWA SHAURINI**

**SWALLOW INVESTMENT (T) CO. LTD POPOTE ULIPO/MLIPO**

**TACH BOARD LTD** Amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo kinondoni (Mwananyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 12/8/2024 saa 03:00 **ASUBUHI/MCHANA MBELE YA Mh. J.W. SILLAS** Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa Saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 24 mwezi 07 , 2024

HABARI KITAIFA

# Wataka maboresho mbinu za kukabili utekaji watoto nchini

**Na Jenifer Gilla**

WIMBI la utekaji wa watoto limeibua wadau wa haki za binadamu na watoto nchini, wakitaka serikali kuboresha mbinu za kukabiliana na vitendo hivyo ikiwamo kuweka mikakati jumuishi.

Wakizungumza na mwandishi wa gazeti hili kwa nyakati tofauti wadau hao walisema kuwa utekaji wa watoto umekuwa ukijirudia licha ya kuwapo sheria zinazokataza.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLCS), Felister Mauya, alisema mwishoni mwa wiki kuwa vitendo vya utekaji watoto ni matokeo ya kudharu na kukiuka Sheria ya Ulinzi wa Mtoto ya Mwaka 2019 inayokataza kumfanyia ukatili wa aina yoyote, vitendo visivyo vya kibinadamu au udhalilishaji wa aina yoyote.

Alisema sababu za kufanya hivyo zipo nyingi ikiwamo biashara haramu ya binadamu, kuuza viungo na wengine kutumikishwa kingono na kutaka fedha kwa wazazi au walezi wao.

Alisema ili kumaliza tatizo hilo wadau wanaotetea haki za jamii wanapaswa kutengeneza mikakati ya pamoja ya kukemea vitendo hivyo katika jamii.

Alitaja mikakati hiyo ni pamoja na kutoa elimu kuanzia ngazi ya familia namna ya kuishi kwa kujihami, ikiwamo kutoa taarifa wanapoona sura ngeni zinazunguka katika mitaa yao bila kuwa na taarifa zao.

Alisema viongozi wa mitaa waelimishwe ili kuhakikisha wanatambua kila mgeni anayehamia katika eneo lake, ikiwamo mahali anapoishi na anapobaini kuna mgeni katika mtaa huo kufuatilia ili kujua dhamira yake.

Mwanasaikolojia tiba, Dk. Saldeen Kimangale, alikumbusha wazazi kuongeza nguvu katika jukumu lao la malezi ili kuhakikisha kuwa watoto wanakuwa katika mikono salama.

Alisema jamii ihamasishwe kufanya kazi kwa bidii ili kupata kipato halali huku akitaka mamlaka za serikali zipunguze changamoto ya ugumu wa maisha unaosababisha watu kutafuta njia za mkato za kufanikiwa.

"Vijana katika ngazi zote za elimu na waliopo nyumbani wafundishe stadi za maisha waweze kutatua changamoto za maisha wanazokabiliana nazo kwa namna bora," alisema. Padre wa Kanisa la Anglikana Kigogo, Joseph Upio alisema wimbi la utekaji ni matokeo ya watu kuacha kutekeleza maagizo ya imani zao na kuweka mbele tamaa za fedha.

Alisema ukifuatilia kwa ukaribu matukio mengi ya watoto kutoweka yanafanywa kwa lengo la kuwanyofoa viungo vya mwili kwa lengo la kuwauzia watu waliotawaliwa na imani za kishirikina na kuwa viungo hivyo vitawapa utajiri.

Alisema cha kusikitisha ni kuwa hata wale watu ambao ni kimbilio katika jamii kama vile viongozi wa dini nao wameingia katika vitendo hivyo, jambo ambalo ni hatari katika jamii.

Alishauri watu wenye nafasi katika jamii kama vile viongozi wa dini, serikalini na waandishi wa habari watumie nafasi yao vizuri kwa kuelimisha jamii kuhusu madhara ya vitendo hivyo.

"Ninyi waandishi wa habari mnapaswa kuwaeleza watu kuwa kisayansi viungo vya binadamu haviwezi kumpa mtu utajiri, huko mitaani kuna taarifa nyingi za upotoshaji na ndio zinachochea haya mambo," alisema.


Air Tanzania Training Centre



KUJIUNGA NA KOZI YAWAFANYAKAZI NDANI YA NDEGE (CABIN CREW)

Chuo cha Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL Training Centre) kinapenda kuwajulisha kuwa kimeanza kupokea maombi ya kujiunga na kozi ya wafanyakazi ndani ya ndege (Cabin Crew). Hii ni maalum kwa wale wote wanaopenda kujiendeleza kitaaluma kwenye kada ya wahudumu ndani ya ndege katika Sekta ya Anga. Kozi hii ni ya muda wa miezi mitatu (03) na masomo yataanza tarehe 01 Oktoba 2024.

**Sifa za mwombaji:**

1. Umri: kuanzia miaka 18 hadi miaka 25
2. Michoro mwilini: Muombaji asiwe na michoro ya kudumu mwilini (tattoos).
3. Muonekano: Awe mwenye akili timamu na mwenye urefu wa kuanzia futi 5"4 (162cm).
4. Elimu: Awe amehitimu elimu ya kidato cha nne na ufaulu angalau wa masomo manne kwa alama "D". Somo la Kiingereza na Jiografia ni lazima.
5. Lugha: Awe na uwezo wa kuongea na kuandika kwa ufasaha Kiswahili na Kingereza. Aidha, muombaji mwenye uelewa wa lugha zingine zaidi za kigeni kama Kiarabu, Kichina au Kifaransa atapewa kipaumbele.
6. Uraia: Awe Mtanzania au raia wa kigeni mwenye vibali halali vinavyomruhusu kusoma nchini. Waombaji kutoka nchi za kigeni watatakiwa kuwasilisha matokeo ya vyeti vyao Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA) ili kupata ulinganifu na matokeo.

**Barua ya maombi:**
Maombi yote ni lazima yaambatishe nyaraka zifuatazo:

1. Nakala ya cheti cha kidato cha nne na vyeti vingine vya shule/chuo alichohitimu.
2. Nakala ya cheti cha kuzaliwa.
3. Picha mbili ndogo (passport size) na picha moja yenye kuonesha umbo lote ukubwa wa 6x8.
4. Wasifu wa muombaji (Curriculum Vitae – CV).

**Kuwasilisha Maombi:**
Wanaopenda kujiunga na kozi hii watapaswa kuwasilisha maombi yao kwa Mkuu wa Chuo, Jengo la Chuo cha ATCL (Ofisi ya Utawala), Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Terminal One, mkabala na Kituo cha Polisi cha Uwanja wa Ndege au kupitia barua pepe: training@airtanzania.co.tz. Maombi yote yatumwe kabla ya tarehe 26 Agosti 2024.

**Anuani:**
**Mkuu wa Chuo, ATCL Training Center**
**S.L.P 543,**
**Dar Es Salaam**
**Kwa maelezo zaidi tafadhali piga: +255754 345 874, +255735 787212.**
**Unayependa kuwa mfanyakazi ndani ya ndege, timiza ndoto yako nasi.**

"TIMIZA NDOTO YAKO KUPITIA CHUO CHA KAMPUNI YA NDEGE YA TANZANIA"


# Wakunga 500 kusomeshwa na benki

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) imesisitiza dhamira yake kufadhili masomo ya wakunga 500 kufikia mwaka 2028.

Ufadhili huo ni sehemu ya mkakati wa benki hiyo katika kuboresha sekta ya afya kupitia uzazi salama na kupunguza vifo vya watoto na kinamama, hususani vinavyosababishwa na uhaba mkubwa wa wataalamu hao.

Dhamira hiyo ilielezwa na Meneja wa benki hiyo tawi la Morogoro, Deusdedit Mashalla wakati akizungumza kwenye Mahafali ya Tano ya Stashahada ya Uuguzi, Ukunga na Teknolojia ya Maabara ya Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Morogoro (MCOHAS), yaliyofanyika chuoni huko mwishoni mwa wiki.

Benki ya NBC ilifadhili masomo ya wakunga 50 kati ya wahitimu 151 wa siku hiyo kwa kushirikiana na Benjamin Mkapa Foundation.

Kwa mujibu wa Mashalla, kupitia makubaliano yake na Taasisi ya Benjamin Mkapa inayoratibu mpango huo, wakunga wanaotarajiwa kupatikana kupitia mpango huo ni wale ambao tayari wako kwenye ajira na watajengewa uwezo zaidi ili wakatoe huduma katika maeneo yenye uhitaji mkubwa wa wataalamu hao nchini.

"Lengo hasa ni kuhakikisha ifikapo mwaka 2028, jumla ya wanufaika wa ufadhili huu inafika 500 ili waende kuokoa maisha ya kinamama na watoto huko kwenye maeneo ya pembezoni kwa kuwa kwa sasa ndio yanakabiliwa na uhaba mkubwa wa wataalamu hawa.

Kwa mujibu wa Mashalla, mpango huo unawezeshwa kupitia mbio za NBC Dodoma Marathon zinazofanyika kila mwaka jijini Dodoma ambapo mbali na kufadhili masomo hayo, mbio hizo pia zimekuwa zinabeba jukumu la kusaidia mapambano dhidi ya saratani ya shingo ya kizazi kwa wanawake kupitia utoaji elimu kwa umma na uchunguzi.

Ni kauli iliyouungwa mkono na Mganga Mfawadhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro, Dk. Daniel Nkungu aliyesisitiza wahitimu hao kuhakikisha wanatumbua lengo kuu la kutoa huduma na kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya fedha.

Mkuu wa Chuo hicho, Evarist Urassa alitoa wito kwa wahitimu hao pamoja na watumishi wengine wa afya kwenye maeneo mbalimbali nchini kuhakikisha wanajiendeleza kielimu mara kwa mara ili kuendana na mabadiliko makubwa ya kitaaluma yanayoendelea kushuhudiwa.

Meneja Uhusiano wa Taasisi ya Benjamin Mkapa Foundation, Mariam Ndabagenga pamoja na kuwapongeza wahitimu, alishukuru NBC kwa ufadhili wa masomo kwa wakunga hao huku akiwasihi wahitimu kuhakikisha wanaonesha tofauti ya kiutendaji kwa kuwa bora zaidi pindi wanaporejea kwenye majukumu yao.

TRA

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

## MAKUSANYO YA KODI KWA MWEZI JULAI 2024 NA MUELEKEO WA UKUSANYAJI MAPATO KWA MIEZI 11 ILIYOBAKI YA MWAKA WA FEDHA 2024/25.

**Dar es Salaam, 09 Agosti, 2024:**

Katika kipindi cha mwezi Julai, Mwaka wa Fedha 2024/25, Mamlaka ya Mapato Tanzania imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi Trilioni 2.34**, sawa na ufanisi wa **asilimia 104.4** ikilinganishwa na lengo la kukusanya **Shilingi Trilioni 2.246**. Makusanyo haya ni sawa na ukuaji wa **asilimia 20.9** ikilinganishwa na **Shilingi Trilioni 1.94** kilichokusanywa katika mwezi Julai kwa Mwaka wa Fedha 2023/24. Ufanisi katika makusanyo na ukuaji wa makusanyo kwa mwezi Julai ni wa juu kabisa kufikiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania katika kipindi cha **miaka sita (06)** iliyopita.

**Jedwali: Makusanyo ya Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa Mwezi Julai, 2018/19 -2024/25**

| Mwaka wa Fedha | Lengo | Makusanyo | Ufanisi | Ukuaji |
|---|---|---|---|---|
| 2024/25 | 2.25 | 2.34 | 104.4% | 20.9% |
| 2023/24 | 2.14 | 1.94 | 90.5% | 9.9% |
| 2022/23 | 1.90 | 1.76 | 93.1% | 14.9% |
| 2021/22 | 1.58 | 1.54 | 97.4% | 19.2% |
| 2020/21 | 1.53 | 1.29 | 84.3% | 2.5% |
| 2019/20 | 1.37 | 1.26 | 91.9% | 4.5% |
| 2018/19 | 1.25 | 1.20 | 96.6% | |

***Shilingi Trilioni***

***CHANZO:*** *Mamlaka ya Mapato Tanzania*

Ufanisi huu umechangiwa na;

i. Kuboresha **mahusiano na walipakodi** kupitia njia ya mawasiliano na majadiliano baina ya viongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na Makundi mbalimbali ya walipakodi;

**ii.** **Kufuatilia na kuchukua hatua za haraka** kwenye vihatarishi vya ulipaji kodi, pamoja na vitendo vya ukwepaji kodi;

iii. Kuongezeka kwa usimamizi wa Watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na kuendelea kuwapatia mafunzo kwa vitendo watumishi wapya kwa lengo la kuongeza uadilifu na weledi katika utendaji kazi wetu;

iv. Kuongeza Usimamizi wa matumizi sahihi ya mashine za EFD na matumizi ya Stempu za Ushuru wa Bidhaa (ETS).

Ufanisi wa makusanyo uliofikiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mwezi Julai ni kiashiria chanya katika kuhakikisha kuwa lengo la makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/25 la **Shilingi Trilioni 30.4** linafikiwa. Katika kufanikisha hili, Menejimenti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania imejipanga kutekeleza kikamilifu mambo yafuatayo:

1. Kutekeleza maagizo yote ya ***Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*** kuhusu usimamizi wa kodi nchini;
2. Kuimarisha mahusiano na ushirikiano na walipakodi pamoja na wananchi wote;
3. Kuimarisha utoaji wa elimu ya kodi na huduma bora kwa walipakodi wote;
4. Kujenga na kuimarisha Mifumo ya Kodi za Ndani na Forodha; IDRAS na TANCIS inayosomana (Interfacing) na mifumo mingine;
5. Kusimamia na kuimarisha misingi ya mfumo mzuri wa kodi, ikiwemo Haki na Usawa katika Utozaji Kodi (No Favouritism or Victimization);
6. Kuimarisha na kusimamia Weledi (Professionalism) na Huduma nzuri kwa Walipakodi (Customer Service) ikiwemo Watumishi wetu wote kuvaa vitambulisho wanapotoa huduma ili kuweka uwazi baina ya mtoa na mpokea huduma;
7. Kusikiliza na kutatua changamoto za kikodi za walipakodi kwa wakati nchi nzima (Taxpayers' Engagement Programs);
8. Kushirikiana na Tume ya ***Mheshimiwa Rais,*** ya Tathmini ya Mfumo wa Kodi Nchini ili kuwa na **Mfumo Rafiki**, unaosimamia usawa, unaorahisisha Shughuli za Kiuchumi na wenye Tija nchini;
9. Kusimamia Utekelezaji wa Makubaliano ya Serikali na Wafanyabiashara nchini ikiwemo uwepo wa Kodi elekezi kwa bidhaa nane zinazoingizwa nchini, pamoja na Mfumo Sahihi kwa Biashara za kuchangia makasha (Consolidation);
10. Kusimamia Uadilifu kwa Watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania na kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria kwa wachache wanaokiuka maadili ya utumishi wa umma;
11. Kukabiliana na vitendo vya ukwepaji Kodi wa kukusudia kwa kuimarisha upatikanaji wa Taarifa hizo na kuendelea kujenga Uwezo na Uadilifu kwa watumishi hususani kwenye ukaguzi na uchunguzi wa Kodi za ndani na kimataifa; na,
12. Kuendelea kurahisisha Shughuli za Kiuchumi Nchini na kuongeza Ulipaji Kodi wa Hiari.

**"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"**

**Yusuph Juma Mwenda**

**<u>Kamishna Mkuu</u>**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi wa soka bado ni tatizo Tanzania Bara

**KILICHOONEKA** katika mechi ya nusu fainali Ngao ya Jamii, ni kwamba ni waamuzi ndiyo waliokuwa na presha na mchezo wenyewe kuliko hata wachezaji.

Wachezaji walikuwa wakicheza kwa kufuata maelekezo ya walimu wao jambo ambalo lilionekana dhahiri machoni mwa mashabiki wa soka waliokuwa wakitazama laivu na wale waliotazama kupitia televisheni. Hawakuwa na presha, walitumia vipaji walivyojaaliwa na mbinu za walimu wao, kiasi cha kuufanya kuwa moja kati ya michezo ya kuvutia kuitazama dabi ya timu kubwa mbili za Simba na Yanga.

Mashabiki walivutiwa na soka lililopigwa kwa pande zote mbili, lakini hawakuvutiwa na baadhi ya maamuzi ya waamuzi, Elly Sasii wa Dar es Salaam, Mohamed Mkono kutoka Tanga, Kassim Mpanga kutoka Dar es Salaam, pamoja na Amina Kyando aliyekuwa mwamuzi wa akiba, akitokea Morogoro, huku mtathmini wao akiwa ni mwamuzi wa kimataifa wa zamani, Soud Abdi kutoka Arusha.

Tuseme tu pamoja na ubora wa mechi yenyewe, lakini haikutendewa haki na waamuzi, hasa Sasii aliyekuwa akionekana akichezesha kwa kutaka 'kutafuta uwiano wa matukio na si kufuata taratibu na sheria 17 za mchezo wa soka duniani.

Tumeshuhudia pande zote mbili zilikuwa zinalalamikia baadhi ya matukio ya mchezo huo, ambayo yalikuwa yakionekana dhahiri kwa refa aliyechezesha ama kwa kutojiamini au kwa woga.

Mara kwa mara tumekuwa tukiliongelea hili kuwa waamuzi wengi wa Tanzania wamekuwa hawajiamini na wamekuwa wakisita kutoa maamuzi magumu pale wanapotakiwa kufanya hivyo.

Haijulikana kama wanakuwa wanakwepa lawama, wanaogopa kuwa vichwa vya habari katika magazeti na simulizi kwenye mitandao ya kijamii au vipi.

Tuseme ukweli tu kuwa pamoja na kwamba soka la Tanzania limekua sana na kusifiwa na mataifa mbalimbali, huku Ligi Kuu ikitajwa kuwa ni ya sita kwa ubora barani Afrika, lakini imekuwa ikififishwa na maamuzi mengi yasiyo sahihi ya waamuzi.

Waamuzi ndiyo wamekuwa ni sumu ya mpira wa Tanzania kutokana na kufanya maamuzi mengi ya kushangaza na hata mara nyingine kuamua matokeo badala ya mchezo wenyewe.

Haiwezekani mtu anafanyiwa madhambi hatua tatu tu kutoka mwamuzi alipo, lakini anakataa kuwa si faulo.

Na hii yote inatokana na tabia ya kutaka kusawazisha kosa kwa kosa ambalo yeye mwenyewe ameliacha mwanzo.

Tunaweza kusema kama hali itakuwa hii, basi waamuzi wa Tanzania bado wana safari ndefu kuchaguliwa kuchezesha michezo mikubwa kama Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), ama michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho barani humu.

Kwa kilichotokea Alhamisi iliyopita, wala haishangazi kuona ni kwa nini waamuzi wetu hawateuliwi kuchezesha mashindano hayo ya Afrika.

Moja kati ya sifa za mwamuzi ni kujiamini na kuchukua maamuzi magumu kwa wakati sahihi, lakini ni kwetu hawapo hivyo.

Tuna wasiwasi hata Video ya Kumsaidia Mwamuzi (VAR), zinaweza zisiwe msaada sana kama hali hii itaendelea.

Huenda mwamuzi akaogopa hata kwenda kwenye video kuangalia marudio ili kufanya maamuzi sahihi.

Na hata akilazimishwa, anaweza kusimamia msimamo wake ule ule hata kama si sahihi kwa sababu pamoja na VAR kusaidia, lakini uamuzi wa mwisho huwa unabaki kwa mwamuzi mwenyewe.

Hapo ndipo tutakuja kugundua kuwa hata VAR yenyewe inaweza isiwe msaada kwetu kama tutaendelea kuwa na waamuzi wa aina hii.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



# Dabi Simba, Yanga sasa inahitaji waamuzi kutoka nje

Na Adam

**TANZANIA** wala si kijiji kilichojitenga hapa duniani, badala yake wananchi wanafuatilia matukio na mambo yote yanayotokea ulimwenguni.

Katika nyanja ya soka, tumekuwa tukiona michezo mkubwa, hasa timu za mahasimu wa nchi au mji mmoja katika mabara mbalimbali duniani zikichezeshwa na waamuzi kutoka nje ya nchi.

Miaka inavyozidi kusonga mbele kwa soka kuwa biashara kubwa, kumekuwa na uhitaji mkubwa wa uwazi wa uhitaji wa waamuzi kutoka nje ya nchi kwenda kuchezesha michezo maalum, ambayo ni ile yenye mvuto kwa mashabiki na mikubwa.

Kwa sasa tunaona dabi kubwa Brazil, Argentina na kwingineko ambako soka limepiga hatua kubwa, zimekuwa zikileta waamuzi kutoka nje ya nchi ambao kazi yao inakuwa ni kuchezesha michezo hiyo tu na wanarudi kwao.

Hapa Afrika, dabi mbalimbali za Afrika Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Rwanda, Misri, Morocco, Tunisia na nyinginezo zimeshaanza kuleta waamuzi kutoka nje kwa ajili ya dabi zao.

Tanzania ambayo ni ya sita kwa ubora wa Ligi Kuu Afrika, bado imeendelea kutumia waamuzi wake wa nyumbani kwa ajili ya michezo hiyo huku kila wakati wakivurunda na kupoteza ladha ya dabi.

Ingeeleweka kama kusingekuwa na matatizo kwenye uchezeshaji wao, lakini kila mechi wanazochezesha zinakuwa na matatizo. Na ukiangalia tatizo la waamuzi wa Tanzania ni woga wa kufanya maamuzi katika matukio yanayotokea dhahiri uwanjani kwa kukwepa lawama na si vinginevyo.

Hili ndilo limesababisha nchi nyingi kuanza kuleta waamuzi kutoka nje ili kuchezesha dabi zao. Zimegundua kuwa wakati mwingine wala si mapenzi ya mwamuzi au rushwa, ila waamuzi ni sehemu ya raia wa nchi hiyo, hivyo anaweza kufanya maamuzi kwa ajili tu ya kujilinda ili aishi kwa amani mtaani.

Kwa maana hiyo hawezi kufanya baadhi ya maamuzi magumu ambayo anaona yanaweza kumfanya asakamwe na kulalamikiwa.

Nadhani hili sasa lianze kuangaliwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF) na bodi yake, kuanzia sasa mechi kubwa, zenye mvuto na kutawalia na hisia kuchezeshwa na waamuzi kutoka nje ya nchi.

> **Tanzania ambayo ni ya sita kwa ubora wa Ligi Kuu Afrika, bado imeendelea kutumia waamuzi wake wa nyumbani kwa ajili ya michezo hiyo huku kila wakati wakivurunda na kupoteza ladha ya dabi.**

Kabla ya kumalizika kwa msimu uliopita, TFF ilisema kuna waamuzi kutoka Sudan wapo nchini na wengine walionekana kuchezesha baadhi ya michezo, hasa wale wa pembeni, sasa nadhani imefika wakati wa kuwaleta wengi zaidi kwa ajili hiyo.

Waamuzi wa Sudan ambao kwa sasa hawachezeshi ligi kutokana na nchi yao kukumbwa na vita ya wenyewe kwa wenyewe, wangeweza kupewa fursa hiyo kuliko Watanzania wenyewe ambao wengine wao wamekuwa wakijirudia kuchezesha mechi hizo, huku wakigawana makosa, kwa sababu kutokana na mara nyingi malalamiko kujitokeza.

Labda nielezee faida za waamuzi kutoka nje wakichezesha dabi. Moja ni kwamba wataaminika na timu zote mbili. Ule ugeni wao ni faida, kwani kwa hisia za timu zote mbili ni kwamba kama anatoka nje ya nchi hatokuwa na mapenzi ya upande wowote. Pili hisia za mashabiki wa Simba na Yanga zitaona si rahisi kula mlungula kwa sababu ni waamuzi wa kimataifa.

Tatu, waamuzi hawa wanaweza kufanya maamuzi magumu na sahihi kwa muda wowote bila kuhofia chochote, kama kusemwa mitaani, kwenye vyombo vya habari, wachambuzi, kwa sababu akishamaliza yeye anaondoka kwenda kwao.

Nne ni kwamba atawafanya hata wachezaji kuwa na nidhamu kwa sababu wanajua ni mwamuzi kutoka nje, moja ya sababu ambazo waamuzi wetu wanapata tabu ni kwamba wachezaji wameshawajua kuwa ni waoga, hivyo wanawatisha na kuwazonga mara kwa mara, licha ya kwamba ni kweli wamefanya makosa.

Na hizi ndizo faida ambazo nchi nyingi kwa sasa wanaowatumia waamuzi kutoka nje kwenye dabi zao, wanazitapa.

Ligi ya sita kwa ubora Afrika, inatakiwa sasa ijiongeze kwa kuleta waamuzi kutoka nje, ili pia kuwalinda waamuzi wa ndani kwa lawama ambazo wakati mwingine zinawafanya wasijiamini.

# Katibu Uenezi ANC kuongoza Bodi Shule Mwalimu Nyerere

**Na Mwandishi Wetu,** KIBAHA

KATIBU wa Uenezi, Elimu ya Umma na Mafunzo wa Halmashauri Kuu (NEC) ya Chama cha African National Congress (ANC) cha Afrika Kusini, David Makhura, amechaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya usimamizi ya Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere (MJNLS) iliyopo Wilaya ya Kibaha, mkoani Pwani.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mkuu wa Shule, Professa Marcelina Chijoriga, alisema kikao hicho kilimchagua Makhura mwishoni mwa wiki kwa kuzingatia vigezo ukiwamo ukweli kuwa moja ya jukumu la msingi la shule hiyo la kutoa mafunzo ya uongozi mahiri katika eneo la siasa kwa viongozi vijana na wa marika mengine ili waweze kuongoza vyama, wamiliki wa shule katika nchi za Afrika Kusini, Zimbabwe, Namibia, Angola, Msumbiji na Tanzania.

"Katika bodi hii ya kwanza ya MJNLS tangu kuanzishwa kwa shule mwaka 2022, wapo viongozi kizazi cha umri mkubwa, umri wa kati na umri wa sasa kama Dk. Frederico George Miranda kutoka Angola mwenye umri wa miaka 35.

Ni kutokana na uhalisia huu ndio maana uenyekiti umekwenda kwa Komredi Makhura huku Waziri Mkuu mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mizengo Kayanza Peter Pinda, akipata imani ya wajumbe kuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi.

Wajumbe wanatoka katika vyama tawala vya ANC (Afrika Kusini), ZANU-PF (Zimbabwe), SWAPO (Namibia), FRELIMO (Msumbiji), MPLA (Angola) na CCM (Tanzania) ambavyo kwa pamoja na Chama cha Kikomunisti cha China (CPC), vinavyomiliki shule hiyo kwa pamoja pia walijikita kutekeleza mambo makuu matatu ambayo ni kupitia, kufanya marekebisho na kupitisha mpango kazi wa shule ikiwa ni pamoja na kalenda ya masomo ya shule kwa kipindi cha mwezi Agosti hadi Desemba, 2024, bajeti ya shule kwa kipindi cha Julai - Desemba, 2024 na kuundwa kwa kamati za bodi ili kurahisisha utendaji wa uongozi wa shule kwa kupunguza utegemezi wa maamuzi yote kutegemea vikao vya bodi.

Kamati zilizoundwa na kupitishwa na kikao cha kwanza cha bodi ni Kamati ya Taaluma na Uendeshaji Shule (AAOC), Kamati ya Fedha na Mipango (PFC) na Kamati ya Utawala, Ukaguzi na Udhibiti Vihatarishi (AGRC).

Kamati zingine ni Rasilimali Watu na Maslahi (HRC) na Taaluma na Usimamizi (AAOC). Wajumbe wengine wa bodi wanaowakilisha vyama vyao katika mabano ni Bendita Lope (FRELIMO) ambaye ni mjumbe wa kamati kuu ya chama hicho, Dk. Frederico George Miranda (MPLA), ambaye ni mkuu wa divisheni inayohusika na sera na mafunzo ya makada katika makao makuu ya chama hicho.

Chama Tawala cha Namibia (SWAPO) mjumbe wa bodi anayekiwakilisha chama hicho ni Dk. Charles Mubita, mwandishi wa habari mkongwe aliyepata kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Utangazaji la Namibia na Dk. Meshack Mpande Sibanda (ZANU-PF), anawakilisha chama tawala cha nchini Zimbabwe huku China ambayo ni mdau mkakati wa shule hiyo ikiwakilishwa na ofisa ubalozi wa ubalozi wa China, nchini Tanzania.




Naibu Katibu Mkuu wa CCM, John Mongella, akibadilishana mawazo na Mkuu wa Shule ya Uongozi ya Mwalimu Nyerere (Mwalimu Julius Nyerere Leadership School), Profesa Marecelina Chijoriga, baada ya kufungua kikao cha kwanza cha bodi ya shule hiyo, Kibaha mkoani Pwani, ambapo David Makhura (wa pili kulia) wa Chama cha African National Congress (ANC) cha Afrika Kusini alichaguliwa kuwa mwenyekiti na Waziri Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda akiukwaa umakamu mwenyekiti wakati wa kikao hicho kilichofanyika mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wabuni mchele unaoondoa vitambi, shinikizo la damu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

HATIMAYE wenye matatizo ya vitambi, ugonjwa wa kisukari, shinikizo la damu (BP), uzito uliopitiliza na wingi wa mafuta mwilini, sasa wanaweza kuondokana na maradhi hayo baada ya kundi la vijana wajasiriamali wilayani Kilombero, mkoani hapa kubuni mchele joto unaoweza kusaidia kumaliza matatizo hayo.

Vijana hao wa Kata ya Kiberege, wilayani Kilombero, walipata ujuzi huo wa kutengeneza mchele joto kupitia mafunzo waliyopatiwa chini ya Mradi wa Skills for Employment Tanzania (SET), yaliyoendeshwa na Shirika la Mtandao wa Vikundi vya Wakulima na Wafugaji Morogoro (MVIWAMORO), chini ya Shirika la Swisscontact kupitia ufadhili wa Ubalozi wa Uswisi, nchini Tanzania.

Mradi huo umelenga kuwafikia vijana wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 24 kuwapatia mafunzo ya ufundi stadi ili waweze kujiajiri au kuajiriwa kuepuka umaskini.

Akizungumza katika mahojiano maalumu katika siku ya kilele cha sherehe za maonesho ya kilimo na wafugaji, Nanenane, yaliyofanyika katika viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere Mjini Morogoro, kiongozi wa kundi hilo, Abiduna Mihalu, alisema wamebuni mchele huo baada ya kupata mafunzo kutoka mradi wa SET katika masuala ya usindikaji na kuongeza thamani vyakula na bidhaa mbalimbali.

Alisema mchele joto, umeongezwa viini lishe toka kwenye ganda la mpunga na kuuondoa mafuta na wanga na kuufanya kuwa na uwezo wa kukabiliana na matatizo ya watu wenye changamoto ya ugonjwa wa kisukari, shinikizo la damu (BP), kupunguza kitambi na uzito uliopitiliza.

"Mtu mwenye kisukari na shinikizo la damu hawezi kula mchele wa kawaida hivyo sisi tumekuja na mbadala wake wa mchele joto ambao tumeondoa mafuta, tumepunguza wanga na kuongeza viini lishe hivyo wenye matatizo ya kisukari, BP, vitambi hii ndio tiba yake," alisema Abiduna.

Fadiya Mohamed aliyenufaika na mradi wa SET, alisema mafunzo mengine waliyopata ni pamoja na kusindika na kuziongezea thamani bidhaa mbalimbali ikiwamo za mihogo, ndizi pamoja na karanga ambazo zimekuwa na soko kubwa na kuwawezesha kujiajiri na kuondokana na umaskini.

Mkurugenzi wa Shirika lisilo la Kiserikali la TESIFA, Jasca Punguti, ambalo linawezeshwa na Shirika la Swisscontact kupitia Ubalozi wa Uswisi nchini Tanzania, alisema shirika hilo limelenga kusaidia kinamama waliotelekezwa na wenza wao kwa kuwajengea uwezo ili kujiajiri pamoja na vijana. Alisema mpaka sasa wameshawasaidia kinamama 170 pamoja na vijana wanaoishi katika mazingira magumu kwa kupata mafunzo bure na wakimaliza wanapewa vifaa kazi bure kwenda kuanzisha ofisi zao.

Ofisa Habari wa Shirika la Swisscontact Tanzania, Masunga Isumbi, alisema mradi wa SET awamu ya pili ulianza mwaka 2022 na hadi kufikia mwaka 2024 wametekeleza miradi 23 iliyolenga kuwafundisha vijana ufundi stadi na maarifa katika kujiajiri au kuajiriwa ikiwa imetekelezwa katika wilaya za Mkoa wa Morogoro kupitia asasi mbalimbali zisizo za kiserikali na sasa wanajielekeza katika mikoa ya Iringa na Mbeya.

Alisema lengo kubwa la mradi wa SET katika kushiriki Nanenane ni kuwapatia nafasi vijana kuonesha bidhaa zao zitokanazo na uzalishaji wao baada ya mafunzo mbalimbali katika sekta za ufugaji wa samaki, kuku, usindikaji vyakula, ushonaji wa nguo na masuala mengine ya ujasirimali ili kuona namna ya kupata uzoefu wa masoko na kujiajiri kuondokana na umasikini.

Maonesho ya Nanenane yamewapatia vijana fursa na nafasi ya kuweza kubadilishana mawazo na uzoefu katika kazi zao, sambamba na kukuta na wafanya biashara na wakulima mbalimbali kutoka maeneo mengine nchi Tanzania, hii imekua fursa kubwa kwa vijana wetu kupata nafasi hii, naamini itachangia kuwa chachu kwao katika kuongeza bidii juu ya kazi zao na kuinua zaidi uchumi wao na familia zao.

Mradi wa SET mkoani Morogoro unatekelezwa katika wilaya za Morogoro Manispaa, Halmashauri ya Morogoro, Gairo, Kilosa, Mvomero, Kilombero, Kilosa, Ifakara na watazidi kufikia maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Morogoro kulingana na uhitaji pamoja na kuendelea zaidi mikoa ya Iringa na Mbeya kupitia ufadhili wa ubalozi wa Uswisi, nchini Tanzania.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Wakulima watakiwa kuchangamkia kilimo cha viungo

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAKULIMA wameshauriwa kuhamasika kwa kuchangamkia fursa ya kupanda miti ya mazao ya viungo ambayo imeelezwa kuwa ni mwarobaini wa tatizo la utunzaji wa mazingira hasa katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye viwanja vya Maonesho ya 30 ya Wakulima 88, Kanda ya Mashariki yaliyofanyika katika Uwanja wa Mwalimu Julius Nyerere, mkoani Morogoro, Ofisa Mwezeshaji wa Mradi wa kuhamasisha jamii kupanda mazao ya viungo unaoendeshwa na Shirika la Kuhudumia Wakimbizi la Tanganyika (TCRS), Alphonce Ngomeni, alisema mradi huo ulianzishwa mwaka 2020.

Alisema mradi huo unatekelezwa katika Kata ya Tawa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro, mkoani hapa na tayari jumla ya wakazi 3,400 wameshagawiwa bure miche 10,500 ya miti ya viungo wakitokea kwenye kaya 1,480.

Ngomeni alisema awali walihamasisha jamii utunzaji mazingira kwa kupanda miti ya vivuli, mbao na matunda katika taasisi mbalimbali za umma zikiwamo shule na zahanati na matokeo hayakuwa mazuri na kwamba wastani wa miti 100 waliyoipanda 20 hadi 40 pekee ilionesha kukua vizuri.

Hata hivyo, Ngomeni alisema wameanza kutoa elimu ya kuongeza mnyororo wa thamani kwa wakulima wa mazao ya ya viungo ikiwamo karafuu ili wauze na kupata faida zaidi kuliko malighafi kwa kampuni na kupata faida kidogo.

Alisema wamekuwa wakigawa miche mbalimbali ya viungo ikiwamo mikarafuu, hiriki, michikichi na korosho, mdalasini na vanila bure, kwa mwaka huu 2024 wamefanikiwa kugawa miche zaidi ya 2000 katika vijiji vya Kifindike, Uponda, Tawa, Mlawilila na maeneo mengine ya Kata ya Tawa.

Aidha, alisema utunzaji wa miti ya viungo ni rahisi kwa sababu mtu anaongeza kipato chake zaidi tofauti na miti mingine na zao kama karafuu humsaidia mkulima kupata Shilingi milioni tano hadi 10 kwa msimu kwa mkulima wa kati ikiwa ana miche 10 baada na kuuza kwa kilo ya Sh. 25,000 hadi 30,000.

Aliitaja faida nyingine kuwa ni mkulima hatumii nguvu kubwa kwasababu huo ni mti ambao anautunza huku akiwa analima mazao mengine kama mahindi.

Naye Katibu wa kikundi cha wakulima wa mazao ya viungo Kata ya Tawa, Mbaraka Thadei, aliishukuru TCRS kwa kuwapa elimu ya upandaji mazao hayo ambayo yamewasaidia kukuza uchumi wao na kuongeza vipato kwenye familia.

Thadei alisema wakiwa wakulima wenye shamba la hekari sita wamefanikiwa kupanda mazao mbalimbali ya viungo na hali ya masoko ipo vizuri na kuwafanya kukua kiuchumi.

# Watanzania 900,000 wanufaika mifuko ya uwekezaji

**Na Beatrice Moses**

WATANZANIA 900,000 kati ya milioni 61.7 wamewekeza maeneo tofauti ikiwamo mfuko wa uwekezaji wa pamoja wa kipato cha ziada kwa kipindi kifupi au kirefu kwa faida ya ukwasi madhubuti.

Mkurugenzi Mtendaji wa Watumishi Housing Investments(WHI), Dk. Fred Msemwa, aliyasema hayo wakati akitoa taarifa ya mwaka ya Mfuko wa Faida Fund kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 23, 2023 iliyotolewa mwishoni mwa wiki kwenye Mkutano Mkuu wa kwanza wa wawekezaji wa mfuko huo uliofanyika jijini Dar es Salaam.

Imeazimiwa kuongeza wigo wa uwekezaji kwa kutoa elimu ya hamasa katika maeneo tofauti nchini ikiwamo vyuoni na vijijini kwa wakulima, kwa kuwa uwekezaji katika mfuko huo ni rahisi unaotumia simu ya mkononi, pia umeunganishwa na mfumo wa malipo ya serikali.

"Faida ya kuwekeza kwenye mfuko huu ni kubwa kwa kipindi cha miezi minane ya mwanzo kilichoishia Juni 20, 2023 ilikuwa asilimia 10 imeendelea kuongezeka hadi kufikia asilimia 12 ya mwaka ulioishia Juni 30, 2024, faida iliyopatikana ni kubwa kuliko kigezo linganifu cha asilimia 9.7 dhamana ya serikali ya miaka mitano," alisema Dk. Msemwa.

Alisema uwekezaji kwenye mfuko huo unaanzia Sh. 10,000, mtu yeyote mwenye kipato kuanzia kidogo, cha kati na juu anaweza kuwekeza na kuvuna faida inayopatikana na inayotokana na thamani ya vipande iliyopo kwenye soko kwa wakati huo.

**Mmoja wa wawekezaji katika mfuko huo, Elizabeth Michael, alisema yeye ni mtumishi wa serikali mkoani Tanga amewekeza kwenye mfuko huo akijiandalia maisha ya kueleweka...**

Mmoja wa wawekezaji katika mfuko huo, Elizabeth Michael, alisema yeye ni mtumishi wa serikali mkoani Tanga amewekeza kwenye mfuko huo akijiandalia maisha ya kueleweka wakati atakapostaafu, anahamasika kwa faida ya gawio anayoiona tangu alipoanza kuwekeza mwaka 2023.

Mwekezaji mwingine Meshack Mafyeko ambaye ni Mkurugenzi wa Voice of Eagle Tanzania alisema wamewekeza na kuhamasisha wasichana waliopo kwenye mradi wa Binti Mwenye Ndoto na uwekezaji kuwekeza kwenye mfuko huo wakiamini kuwa itawasaidia kukua kiuchumi siku zijazo.

Mwalimu wa masuala ya fedha, Amina Ramadhani, alisema kuna haja ya kuwahamasisha vijana kuwekeza kwenye matumizi mazuri ya fedha, ikiwamo kwenye kumiliki vipande vya mifuko ya aina Faida Fund, kwa kuwa inaaminika hivyo ni salama badala ya kutumia fedha zao kwenye mambo yasiyowaletea maendeleo ya kiuchumi.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya WHI, Abdul-Razaq Badru, alisema ongezeko la ukuaji wa mfuko huo linatokana na ongezeko la idadi ya wawekezaji kwa kipindi kinachoishia Juni 31, 2023 ilifikia 2,041 hadi Juni 2024 imefikiwa wawekezaji 4,806 sawa na ongezeko la asilimia 58.

"WHI itaendelea kutekeleza mipango yake ikiwamo kuboresha mfuko na huduma kwa wawekezaji, pamoja na kubainisha fursa nyingine za kibiashara kwa manufaa ya wawekezaji na serikali pamoja na wadau wengine.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Reliance, Ravi Shankar (kulia), akimkabidhi madawati 150 yenye thamani ya Sh. milioni 8 Ofisa Elimu ya Awali na Msingi wilayani Mafia, mkoani Pwani, Mathew Mkali (kushoto), yatakayopunguza uhaba katika Shule ya Msingi Kiegeani. Wanaoshuhudia katikati ni Mkurugenzi wa Bodi wa Kampuni hiyo, Anver Rajpar na Mkurugenzi wa Kampuni ya African Overseas, Khairunbanu Alibhai. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi 100 kwenda masomoni ughaibuni

**Na Joseph Mwendapole**

WANAFUNZI 100 wanaondoka wiki hii kwa ajili ya masomo kwenye vyuo vikuu mbalimbali duniani.

Hiyo inakuja ikiwa zimepita wiki mbili tangu matokeo ya kidato cha sita kutoka huku mamia ya wanafunzi wa Tanzania wenye kuhitaji kusoma nje ya nchi kupitia Wakala wa Elimu Nje ya Nchi Global Education Link (GEL) wameanza maandalizi ya kuondoka.

Mkurugenzi wa GEL, Abdulmalik Mollel, alisema hayo wakati akigawa Viza 100 kwa wanafunzi wanaotarajiwa kuondoka Jumatano na pia alizungumza na wazazi na wanafunzi wanaotarajiwa kwenda nchi mbalimbali kimasomo.

Mollel alisema lengo la mkutano huo ilikuwa ni kukabidhi Viza, kujadili na wazazi na wanafunzi kuhusu mambo mambo ya kuzingatia katika maandalizi ya safari, kuwakutanisha wazazi na wanafunzi na wawakilishi wa vyuo vikuu ambavyo wanafunzi hao wanatarajia kwenda kusoma pamoja na kujaza nyaraka mbalimbali.

"Leo tumekutana na wanafunzi hawa kuwapa viza zao ambazo zimekamilika, kuwapa bima za afya kuwaeleza tarehe za kusafiri, ndege watakazotumia kusafiria, kujua sehemu watakazokaa, watasafiri na nani na watapokewa na nani," alisema Mollel.

"Wataanza kuondoka kwenda kwenye vyuo vikuu mbalimbali duniani kuanzia wiki ijayo na baada ya hapo kila wiki kundi la wanafunzi kuanzia 50 mpaka 70 watakuwa wanaondoka kwenda mataifa mbalimbali," alisema Mollel.

Aliwataka wanafunzi kuzingatia walichofuata nje ya nchi na kuachana na starehe na badala yake wazingatie masomo na kuhitimu wakiwa na alama nzuri ili kuwapa moyo wazazi ambao wanajinyima kwaajili ya kuwalipia ada.

Alisema baadhi ya wanafunzi wana kawaida ya kufanya mambo yanayosababisha washindwe kumaliza masomo yao na kuwakatisha tamaa wazazi wao.

"Msiende kunywa pombe wala kwenda klabu za usiku kwasababu kule mnakwenda kufuata elimu. Malizeni masomo mpate kilichowapeleka starehe hata Tanzania zipo," aliasa Mollel.

Aiman Mohamed kutoka Mwanza ambaye anatarajia kwenda masomoni nchini India wiki ijayo, alisema anashukuru uratibu uliofanywa na Global Education Link na kumwezesha kupata Chuo cha Sharda cha nchini humo.

"Kwa dhati kabisa nawapongeza waratibu wa safari yetu Mollel na wenzake kwa namna walivyokuwa karibu na sisi wakati wote wa kuratibu safari na hatimaye mambo yamekuwa mazuri na wiki ijayo tunasafiri kwenda masomoni kutimiza ndoto zetu," alisema.

Rita Nichalaus kutoka Mwanza anayetarajia kujiunga na Chuo Kikuu cha Sharda, New Delhi, India alisema amefurahi kupata elimu ya mambo ambayo wanatakiwa kufanya na ambayo hawatakiwi kuyafanya wanapokuwa masomoni.

"Mwongozo tuliopewa ni muhimu sana kwasababu mwanafunzi anapofika ugenini asipofahamu tabia na tamaduni za wenyeji anaweza kujikuta yuko matatizoni, lakini tumeelezwa namna ya kuishi tukiwa huko ni jambo jema na la msingi sana kwetu," alisema.

HABARI KITAIFA

# Nsekela: Tunakusudia kufanya Ushirika ujiendeshe kibiashara

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MWENYEKITI wa Kamisheni ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Abdulmajid Nsekela amesema ndani ya miaka miwili ya kamisheni hiyo kutekeleza majukumu yake, kipaumbele chake ni kufanya Ushirika nchini ujiendeshe kibiashara ili kunufaisha zaidi wanachama wake.

Nsekela ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, alisema hayo wakati wa mkutano wa maofisa ugani pamoja na viongozi wa vyama vya ushirika kutoka halmashauri zote nchini ulioitishwa na Rais Samia Suluhu Hassan na kufanyika Ikulu ya Chamwino, Dodoma mwishoni mwa wiki iliyopita.

"Tunaendelea kuvijengea uwezo vyama vyetu vya ushirika katika maeneo mbalimbali ili viweze kujiendesha kibiashara. Maeneo hayo ni pamoja na ufugaji na ujenzi wa viwanda vipya ili kuongeza thamani ya mazao ya wakulima na utambuzi na uthaminishaji mali za vyama vya ushirika. "Vilevile, tunahimiza uwekezaji katika dhamana za serikali, ununuzi wa hisa za kampuni, uagizaji na usambazaji pembejeo kwa wanaushirika na wakulima pamoja na ujenzi wa maghala," alisema Nsekela.

Mwenyekiti huyo alisema wanafanya hivyo ili kubadili mtazamo wa kufanya kazi kwa kutoa huduma pekee ili vyama hivyo vinufaishe wanaushirika kwa kuwaletea maendeleo kupitia faida inayopatikana kutokana na uendeshaji vyama vyao kibiashara.

Ndani ya kipindi hicho cha miaka miwili ya kuwapo kwa TCDC, Nsekela alisema wamevifanyia kazi vipaumbele saba vinavyolenga kuboresha mazingira ya wakulima, wafugaji na wavuvi pamoja na wanaushirika kutoka sekta nyingine ambako hamasa ya kujiunga inaendelea kutolewa.

Vipaumbele vingine, Nsekela alivitaja kuwa ni kuhakikisha ushirika unaendeshwa kidijitali kwa kuwa tayari wamefunga Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) unaotumika kuendesha shughuli zote za TCDC, hali iliyorahisisha upatikanaji taarifa na takwimu halisi.

Hadi mwishoni mwa Juni 2024, alisema mfumo wa MUVU umesajili vyama 6,361 vya pamoja na wanachama 1,604,224 wa ushirika. Kipaumbele kingine alisema ni kuhamasisha ushirika kwenye sekta mbalimbali za kiuchumi zikiwamo madini na fedha pamoja na makundi maalum.

Alisema tume pia inakuza ushirikiano na wadau mbalimbali wa maendeleo kwa lengo la kusaidia kuimarisha Ushirika nchini.

**Kingine kilichofanywa na kinachoendelea kupewa msisitizo, Nsekela alisema ni mapitio na mabadiliko ya Sera ya Ushirika ili kuifanyia mabadiliko Sheria ya Vyama vya Ushirika**

Kingine kilichofanywa na kinachoendelea kupewa msisitizo, Nsekela alisema ni mapitio na mabadiliko ya Sera ya Ushirika ili kuifanyia mabadiliko Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya Mwaka 2013.

Alisema tayari hatua zote muhimu zimekamilika na Wizara ya Kilimo inasimamia kupeleka muswada husika bungeni.

Ili kuwa na nguvu ya kiuchumi, Nsekela alisema TCDC imekamilisha utaratibu wa kisheria wa kuanzisha Benki ya Taifa ya Ushirika Tanzania na tayari wameshapata leseni kutoka Benki Kuu ya Tanzani (BoT) ili kuianzisha.

"Mheshimiwa Rais, matarajio ni kuizindua benki hii mwishoni mwa mwezi Septemba 2024 ili kuanza shughuli zake. Na tumeomba kupitia kwa Mheshimiwa Waziri wetu wa Kilimo kuwa, wewe Mheshimiwa Rais, uwe mgeni rasmi katika tukio hilo muhimu," alisema Nsekela.

Benki ya CRDB imewekeza mtaji wa Sh. bilioni 10.2 na utaalamu ndani ya Benki ya Ushirika Tanzania itakayozinduliwa mwezi ujao, ikitarajiwa kumiliki asilimia 20 ya hisa zake. Uwekezaji huo umefanywa kwa kutoa fedha za kunusuru benki za Kilimanjaro Cooperative Bank (KCBL) na Tandahimba Cooperative Bank (Tacoba) kutokana na kutofanya vizuri mpaka zikaimarika. Benki hizi zitakuwa sehemu ya Benki ya Taifa ya Ushirika Tanzania.

Kipaumbele kingine, Nsekela alisema ni kuimarisha uwekezaji wa mali za Ushirika kwa kuwa tume imeratibu utambuzi wa mali zote za vyama vikuu vya ushirika pamoja na SACCOS Daraja B.

Kwa tathmini iliyofanywa kwenye vyama 610 vya ushirika, wamegundua vina mali zenye thamani ya Sh. trilioni 4.2, hivyo kuingizwa katika mfumo wa MUVU.

Akihutubia washiriki wa mkutano huo, Rais Samia alisema sekta ya kilimo ni muhimu sana kwa usalama wa chakula na maendeleo ya Watanzania, hivyo anatambua majukumu makubwa waliyonayo maofisa ugani na mchango wa Ushirika nchini ndio maana ametenga muda wa kukutana na wawakilishi wake kutoka kote nchini.

Rais alisema umuhimu wa vyama vya ushiriki nchini unaanzia kwenye harakati za ukombozi wa taifa na kuandaa viongozi wa kitaifa waliolitumikia taifa mara tu baada ya uhuru.

Kutokana na ukweli huo, Rais Samia alisema anaamini Tanzania inao uwezo wa kulisha Afrika na kutoa mchango mkubwa duniani, hivyo akasisitiza maofisa kilimo kutekeleza wajibu wao wa kuwasaidia wakulima kulima kisasa huku serikali ikitimiza haki zao.



Meneja wa Benki ya NBC tawi la Morogoro, Deusdedit Mashalla (katikati aliyevaa joho), akishuhudia baadhi ya wahitimu wa Stashahada ya Ukunga katika Chuo cha Afya na Sayansi Shirikishi Morogoro (MCOHAS) wakionesha namna ya kuhudumia mama na mtoto wakati wa kujifungua wakati wa mahafali ya tano ya chuo hicho mwishoni mwa wiki. Wahitimu hao ni miongoni mwa wanufaika 50 wa ufadhili wa masomo ya ukunga uliotolewa na benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni tuhuma kuchinja mwenye ulemavu

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

JESHI la Polisi mkoani Manyara linamshikilia Amos John (29) kwa tuhuma za mauaji kwa kumchinja Fatuma Said (28) aliyekuwa anaishi naye.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) George Katabazi, Fatuma alikuwa na ulemavu. Alisema tukio hilo lilitokea Agosti 9 mwaka huu na wanamshikilia mtuhumiwa huyo.

Kamanda Katabazi alisema mtuhumiwa huyo anadaiwa kutumia kitu chenye ncha kali kumchinja Fatuma na wanaendelea na mahojiano naye kuhusu tukio hilo.

"Chanzo halisi cha mauaji haya hakijajulikana ila uchunguzi wa awali unaonesha kuwa Amos alikuwa amekunywa pombe na kusababisha kutenda mauaji hayo," alisema Kamanda Katabazi.

Watu wenye ulemavu katika Mji wa Mirerani, wilayani Simanjiro mkoani hapa wamelaani tukio hilo.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu Wilayani Simanjiro, Robert Matheus, akizungumza na waandishi wa habari jana, alisema wamesikitishwa na tukio hilo.

Alisema wamesikitishwa na kitendo cha mwenzao kudaiwa kuuawa kwa kuchinjwa shingoni na mwanamume aliyekuwa anaishi naye. "Huyu dada alikuwa ulemavu wa mguu na mkono na alikuwa mpambanaji lakini huyu mwanamume amekatisha ndoto yake aliyokuwa nayo," alidai.

Ndugu wa marehemu, Elihuruma Eliafia, alisema Fatuma ni mama yake mdogo huku mama mwenye nyumba alikokuwa anaishi Fatuma, Upendo Swai, akisema kuwa Agosti 9 mwaka huu, alisikia kelele zikitoka katika chumba cha wawili hao.

Alisema: "Nikamwuliza huyo mwanamume aliyekuwa anaishi naye, hii damu ya nini, mbona Fatuma haonekani? Akadai kuwa 'Fatuma anaumwa na damu zinamtoka puani'."

# 'Wasichana jitokezeni kugombea 2024, 2025'

**Na Elizabeth Zaya**

SHIRIKA la Msichana Initiative limehimiza wasichana kujitokeza kuwania nafasi za uongozi katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani.

Uongozi wa shirika hilo unaamini hiyo ni fursa nzuri kwa wasichana kusimamia na kutetea ajenda zao endapo watafanikiwa kuchaguliwa.

Msimamizi wa Mradi wa Sauti Yetu, Nguvu Yetu ulio chini ya shirika hilo, Rose Batoba, alitoa rai hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa semina ya kuwajengea uwezo wasichana kutoka mikoa mbalimbali nchini iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Rose alisema miongoni mwa mambo wanayowajengea uwezo wasichana hao ni kujitambua kukabiliana na vitendo vya unyanyasaji ikiwamo rushwa ya ngono hususani katika kipindi cha uchaguzi.

"Kwa hiyo, tunawajengea uwezo namna ya kuwa viongozi, kujitambua kukabiliana na vitendo mbalimbali vya unyanyasaji na kuweka nguvu katika kufikia malengo yao katika uongozi," alisema Rose.

Mmoja wa wasichana waliojengwa uwezo na shirika hilo, Mwajuma Hima kutoka wilayani Ubungo, alisema tayari wameshaanza kazi ya kuhamasisha wasichana kupitia makundi yao mbalimbali na wako tayari kugombea nafasi katika uchaguzi wa mwaka huu na mwakani.

"Wasichana wote wa Tanzania hatutakiwi kufungiwa ndani, tuna nguvu na tuna uwezo wa kusimama katika nafasi yoyote ya uongozi. Hivyo, katika uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu, tujitokeze kwa wingi twende tukagombee nafasi hizo ni zetu na itakapofika mwaka kesho, nazo ni zetu tutajitokeza," alisema Mwajuma.

Loveness Athuman kutoka Nzega, mkoani Tabora, alisema kuwa hivi sasa shirika hilo limekuja na programu ya kipekee ambayo inasaidia wasichana hao pamoja na mambo mengine kushiriki nafasi za uongozi na kuondoa imani ya kwamba mtoto wa kike hawezi kuwa kiongozi.

Walter Charlos, Mwanachama wa Mtandao wa Katiba, Wanawake na Uongozi pamoja na Uchaguzi, alisema mifumo ya kijamii pamoja na mila na desturi kandamizi ni changamoto kubwa zinazochangia wanawake wasijitokeze kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.





# Ajali ya gari yaua watatu wa familia moja

**Na Vitus Audax,** SIMIYU

WATU watatu wa familia moja waliokuwa wakisafiri katika mkokoteni uliokuwa ukikokotwa na ng'ombe wamefariki dunia baada ya basi la kampuni ya Ally's kugongana na gari aina ya fuso katika Kijiji cha Ruguru wilayani Itilima mkoani Simiyu. Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Edith Swebe, amethibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kusema ilitokea juzi katika kijiji hicho, kutaja waliofariki dunia ni Ngusa Mbesi (24), Sende Mbese (7) na Kisamo Mbesi (9). Kamanda Edith alisema katika ajali hiyo pia ng'ombe sita walifariki hapo hapo.

Aidha, alisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi wa dereva aliyekuwa akiendesha fuso ambaye hakuchukua tahadhari. Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya mashuhuda walieleza kuwa chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa fuso kupishana na gari la mbele yake bila kuchukua tahadhari.

**"Alilipita gali la mafuta lililokuwa mbele yake ambalo tayari lilikuwa limeishafika darajani na kusababisha ajali hiyo," alisema manusura Abdulmaliki Samwel.**

"Alilipita gali la mafuta lililokuwa mbele yake ambalo tayari lilikuwa limeishafika darajani na kusababisha ajali hiyo," alisema manusura Abdulmaliki Samwel.

Alisema dereva wa basi walilokuwa wamepanda baada ya kuona fuso hilo likija upande wake alijaribu kulipisha lakini likaligonga na kupoteza uelekeo na kuelekea walikokuwa wakiendesha mkokoteni uliobeba ng'ombe na baadhi ya watu. Shuhuda mwingine, Masanja Masunga alisema baada ya basi hilo kuwagonga waendesha mkokoteni, mkokoteni huo uliburuzwa uvunguni mwa basi hilo hadi upande wa pili.



Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, akizungumza na vijana kutoka mikoa mbalimbali hapa nchini wanaodaiwa kutapeliwa kupewa ajira na kupokonywa nyaraka zao za elimu alipofanya ziara ya kushtukiza katika ofisi zao zilizoko Kata ya Nyihogo-Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga jana. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Sababu ongezeko watoto wenye utapiamlo Kahama yatajwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

ONGEZEKO la watoto wanaoachishwa kunyonywa kabla ya wakati wilayani Kahama mkoani Shinyanga imetajwa kuwa chanzo cha ongezeko la watoto wenye utapiamlo na udumavu.

Pia, imetajwa kusababishwa na ukosefu wa elimu sahihi ya unyonyeshaji kwa wananchi, hali inayosababisha kuanza kuwalisha watoto vyakula mbalimbali kama mbadala wa maziwa.

Hayo yamebainishwa juzi na Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Ushetu, Khadija Nasibu wakati akizungumza na wananchi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Lishe yaliyofanyika katika Kijiji cha Uyogo na kuahidi kuendelea kuwafikia wananchi ili kuwapa elimu ya lishe kwa mtoto.

Alisema wastani wa watoto wanne hadi watano kati ya 10 wananyonyeshwa kwa miezi sita pekee ya mwanzo, sehemu kubwa ya watoto hao hupewa maji wakiwa na miezi miwili na wengine kuanzishiwa maziwa na kuachwa kunyonyeshwa tena.

Alisema hali hiyo inasababisha kuwa na ongezeko la watoto wenye lishe duni.

Khadija alisema watakuwa wanatoa elimu hiyo hasa wakati wa kliniki ambayo itaambatana na makundi ya vyakula vyenye lishe kwa watoto ili kutambua namna sahihi ya kuandaa chakula hicho na kuwataka wajawazito na wenye watoto wadogo kuhakikisha wanahudhuria kliniki vipindi vyote.

Kaimu Mganga Mkuu wa Hospitali ya Ushetu, Dk. Jenviva Gabriel alisema wengi wao wamekuwa wakiacha kunyonyesha watoto na kukimbilia shambani kulima wakati mtoto anahitaji maziwa ya mama ili kukomaza ubongo.

Hivyo, aliwataka kuzingatia suala la unyonyeshaji kama ambavyo wamekuwa wakikumbushwa wawapo kliniki.

Alisema mtoto asiyenyonyeshwa ipasavyo anakuwa hana uwezo wa kutunza kumbukumbu na kile atachokuwa anafundishwa awapo shuleni hakitakuwa kinakaa akilini na mwisho wake atashindwa kufanya vema kwenye masomo yake.

Mkazi wa Kijiji hicho, Amina Mussa alisema, miaka ya nyuma walikuwa wakinyonyesha watoto mpaka miaka mitatu na wakati mwingine walilazimika kuwaachisha watoto kwa nguvu lakini vijana wa sasa wananyonyesha ndani ya miezi sita mpaka mwaka mmoja.

# TFRA yaagizwa kutoa elimu matumizi ya mbolea

**Na Renatha Msungu,** MWANZA

MWENYEKITI wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Dk. Antony Diallo, ameiagiza TFRA kuelekeza nguvu katika uelimishaji wa matumizi ya mbolea kwenye zao la pamba na mazao mengine ili kuinua uchumi wa wakulima.

Alitoa agizo hilo juzi baada ya maonesho ya Nanenane na kueleza kuwa wakulima wengi wako nyuma kwenye matumizi ya mbolea, hivyo elimu inahitajika ili waongeze kiwango cha mavuno kwenye zao hilo.

Alisema pamba ni zao la biashara ambalo huwaingizia kipato wakulima wa Kanda ya Ziwa lakini msukumo wao katika kutumia mbolea umekuwa chini hali inayorudisha nyuma kiwango cha uzalishaji.

Meneja wa TFRA Kanda ya Ziwa, Michael Sanga, alisema wanaendelea na utoaji elimu, huku akisisitiza kuwa watazingatia maagizo yaliyotolewa.

Alisema malengo walionayo ni kuhakikisha wakulima wanatumia mbolea na kuondokana na kilimo cha mazoea katika maeneo mbalimbali.

Baadhi ya wakulima akiwamo, Nyanda Zuberi alisema serikali iongeze nguvu kwenye suala la utoaji wa mbolea ya ruzuku ili imfikie kila mkulima na kuwasaidia katika kukuza uzalishaji katika kilimo.

Alisema mbali na mbolea hiyo pia wahimize wakulima kujiandikisha ili kupata mbolea ya ruzuku kwa urahisi na siyo kwenda kununua kwa kulanguliwa.

# Mradi Ziwa Victoria waleta neema wakazi 15,000

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

WANANCHI zaidi ya 15,000 kutoka katika vijiji vya Seseko na Ngundangali wilayani Kishapu mkoani Shinyanga wameanza kunufaika na huduma ya majisafi na salama kutoka katika Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria. Wakizungumza juzi baada ya uzinduzi wa mradi huo uliofanywa na Mwenge wa Uhuru wenye mtandao wa bomba la kilomita 41.5 baadhi ya wanawake wa vijiji hivyo waliishukuru serikali kwa kukamilisha mradi huo na kuwaondolea adha ya kutafuta maji umbali mrefu.

Meneja Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) Wilaya ya Kishapu, Dickson Kamazima alisema umekamilika kwa asilimia 100 na tayari umeshaanza kutoa huduma kwa wananchi katika vijiji hivyo viwili.

"Mradi huu chanzo chake cha maji ni Ziwa Victoria na gharama zake ni Sh. bilioni 2.8 na wananchi wapatao 15.500 watanufaika," alisema Kamazima.

Naye kiongozi wa mbio za Mwenge wa Uhuru Taifa, Godfrey Mnzava, akizungumza wakati wa kuzindua mradi huo aliwataka wananchi kuitunza miundombinu ya maji pamoja na vyanzo vya maji, ili iendelee kuwahudumia kwa muda mrefu na kutatua adha ya ukosefu wa majisafi na salama katika maeneo yao.

Nipashe
Spotika



TIMU ZINAZOWEZA KUIZUIA MAN CITY KUTWAA UBINGWA WA EPL UK. 12



Sancho

# MAWINGA WATANO WANAOIFAA BARCA KAMA IKIMKOSA WILLIAMS

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA inaweza kuwa na ndoto ya kumsajili Nico Williams, lakini kila kukicha inazidi kuwa wazi huenda hawatampata mchezaji huyo.

Dhamana ya Williams kwa Athletic Club bado ni imara na ni vigumu na hiyo ni klabu yake ya utotoni.

Muda wote wa kiangazi, rais wa Barca, Joan Laporta, ameshikilia kuwa klabu hiyo ina fedha za kumnunua Williams kwa kifungu chake cha euro milioni 60 cha kuachiliwa.

Dani Olmo tayari ameigharimu Barcelona kiasi sawa na hicho baada ya dili kuafikiwa na RB Leipzig na bado haijajulikana kama hilo litatoka kwenye bajeti ya Williams.

Lakini tuseme sivyo hivyo na 'La Blaugrana' hao wana euro milioni 60 kumtupia winga kufanya kazi pamoja na Lamine Yamal. Je, wakimkosa huyo wamlenge nani?

Hapa tunawaangalia mawingia watano wanaoweza kuwafaa Barcelona, haya sasa...

**#1. Jadon Sancho**

Ingawa Erik ten Hag amemkaribisha Jadon Sancho, Manchester United bado wanaweza kumuuza winga huyo kabla ya dirisha la usajili kufungwa.

Kwa sababu moja au nyingine, haijafaulu kwa Sancho katika nchi yake ya asili ya England, na ingawa ilimchukua muda kwenda katika kipindi cha pili cha msimu uliopita akiwa kwa mkopo Borussia Dortmund, kiwango chake cha Ligi ya Mabingwa kilithibitisha kuwa yuko na bado ni winga mwenye heshima.

Sancho tayari amekuwa akihusishwa na Barcelona dirisha hili, lakini si sana tangu Williams awe shabaha yao kuu.

**#2. Kingsley Coman**

Bayern Munich wanatazamia siku zijazo - Michael Olise amejiunga kutoka Crystal Palace, na mazungumzo yanaendelea kuhusu Desire Doue wa Rennes.

Kwa kiongozi mkuu kama Kingsley Coman, lazima awe anashangaa nini kitatokea katika klabu hiyo. Je, ataaminiwa kucheza chini ya kocha mkuu mpya Vincent Kompany? Je, atapewa nafasi nyingine mbele ya nyota wa kesho?

90min ilifichua mapema msimu huu wa joto kwamba Bayern wangekuwa tayari kumuuza Coman kwa euro milioni 50 na Barcelona walikuwa miongoni mwa timu zinazofuatilia hali yake. Ikiwa Williams atashindwa, ni vigumu kufikiria kwamba hawatachunguza tena hatua hii tena.

**#3. Mathys Simu**

Iwapo Barcelona wanataka mbadala wa Coman mwenye umri mdogo zaidi, basi pengine inafaa kumtafuta fowadi mwenye umri wa miaka 19, Mathys Tel.

Kuna uwanja mzuri ambao Barca wanaweza kuweka mbele, pia. Jarida la ol' 'Barca DNA' likipamba kwenye vyombo vya habari vya Katalunya, likitilia shaka umuhimu wake kwa mradi wa Bayern huku Wafaransa wenzake Olise na Doue wakiendesha safu za ulinzi.

Bayern walijaribu kumaliza uvumi juu ya mustakabali wa Tel kwa kumsainisha mkataba mpya Machi mwaka huu. Lakini kama tumejifunza katika soka, hiyo haijalishi ikiwa mchezaji amedhamiria kuhama.

**#4. Federico Chiesa**

Juventus wameweka wazi kuwa Federico Chiesa anaweza kuondoka msimu huu wa majira ya joto, na ripoti nchini Italia zinadai kuwa watakuwa tayari kukubali ombi la chini la euro milioni 20.

Ni kweli kwamba historia ya utimamu wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, si nzuri, na kumweka katika kikosi cha Barcelona cha kupata majeraha hakuwezi kuboresha bahati yake. Lakini ikiwa La Blaugrana wanatamani sana, inafaa kulipwa kwa bei hiyo, sivyo?

**#5. Pedro Neto**

Sifa moja ambayo wachezaji wengine wanne kwenye orodha hii wanafanana ni kwamba wana miguu ya kulia, kwa hivyo Pedro Neto yuko hapa kama msafishaji.

Akiwa na uwezo wa kucheza popote kwenye mstari wa mbele na kujivunia uzoefu wa kimataifa, Neto angefaa mtindo maarufu wa Barcelona na kuleta upana wanaoutamani.

Hivi majuzi Neto alidai kuwa alikuwa na furaha akiwa Wolves.

## ISIKUPITE

WACHEZAJI wa Man City walionesha kiwango bora zaidi kwenye mchezo wa Ngao ya Jamii dhidi ya Man United juzi ni Oscar Bobb - 8/10 na Rico Lewis - 8/10, aliyeonesha kiwango cha chini zaidi ni Josko Gvardiol - 5/10. Kwa upande wa Man United ni Alejandro Garnacho - 8/10 na Amad Diallo - 7/10, waliovurunda zaidi kwa United ni Jonny Evans - 4/10 na Diogo Dalot - 5/10.





# TIMU ZINAZOWEZA KUIZUIA MAN CITY KUTWAA UBINGWA WA EPL

Wachezaji wa Arsenal

**LONDON, England**

SWALI la kila mwaka ni hili - kuna timu yoyote inayoweza kuizuia Manchester City kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu England, EPL?

Kwa msimu wa tisa mfululizo kikosi hicho cha Kocha Pep Guardiola kinapewa nafasi kubwa ya kutwaa taji la Ligi Kuu England.

Wameshinda mataji sita kati ya saba yaliyopita, yakiwamo manne mfululizo.

BBC Sport inazitazama timu saba, wapinzani wa Man City wenye uwezo pia wa kutwaa taji. Timu zimepangwa kulingana na nafasi zao za kumaliza msimu uliopita, twende sasa...

**Arsenal**

Mwisho wa msimu uliopita, walikuwa nafasi ya pili, pointi mbili nyuma ya City. Wamemaliza washindi wa pili chini ya Man City katika misimu miwili iliyopita.

'Washikabunduki' wa London hao wamefanya mabadiliko makubwa, wamemleta mlinzi wa Italia, Riccardo Calafiori kutoka Bologna kwa ada ya pauni milioni 42. Anaweza kucheza beki wa kushoto au wa kati.

Pia wamegeuza mkataba wa mkopo kuwa wa kudumu kwa kipa wa Hispania, David Raya, ambaye alimpiku Aaron Ramsdale na kuwa namba moja msimu uliopita.

Winga Bukayo Saka ndiye mfungaji wao bora katika misimu miwili iliyopita. Na wanahusishwa kutaka kumnunua mshambuliaji wa Napoli, Victor Osimhen.

"Nahodha wa Arsenal, Martin Odegaard, alisema mwishoni mwa msimu uliopita kwamba, wameibadilisha klabu na anaamini Arsenal watashindania taji kwa muda mrefu," anasema Mwandishi wa Michezo wa BBC, Alex Howell.

**Liverpool**

Mwisho wa msimu walikuwa nafasi ya tatu, pointi tisa nyuma ya Man City. Liverpool wanaanza msimu bila ya Kocha Jurgen Klopp kwa mara ya kwanza tangu 2015-16.

Klopp alitangaza ataondoka mwishoni mwa msimu, lakini tangazo lake lilikuja katikati ya msimu uliopita - na nafasi yake imechukuliwa na Arne Slot, Mei mwaka huu.

Mholanzi huyo anaonekana kubadilisha mtindo wa uchezaji wa Liverpool kutoka mchezo wa nguvu na haraka hadi ule wa kumiliki mpira.

Liverpool ndio timu pekee mbali na Man City kushinda taji la Ligi Kuu katika kipindi cha miaka saba iliyopita, bado hawajasajili mtu yeyote msimu huu - lakini Slot anatumaini watasajili.

Mwandishi mwandamizi wa soka wa BBC Sport, Nizaar Kinsella, anasema: "Liverpool wanatarajia kuleta ushindani katika msimu wa kwanza wa Slot baada ya enzi nzuri chini ya Jurgen Klopp na kuiacha klabu katika nafasi nzuri."

**Aston Villa**

Mwisho wa msimu uliopita walikuwa nafasi ya nne na pointi 23 nyuma ya Man City. Ilifuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa kufanikiwa kumaliza katika nafasi ya nne msimu uliopita.

Unai Emery ameigeuza klabu hiyo kutoka kugombea kutoteremka daraja hadi timu ambayo inazungumzwa kama mshindania taji msimu uliopita - na hata hajaiongoza kwa miaka miwili bado.

Klabu hiyo inalazimika kuuza wachezaji msimu huu wa majira ya joto ili kutimiza kanuni za faida na kifedha za Ligi Kuu England.

Lakini wameleta sura nyingi mpya - ikiwa ni pamoja na kiungo wa Everton. Amadou Onana, beki wa kushoto wa Chelsea, Ian Maatsen, kiungo wa kati wa Luton, Ross Barkley - na vijana wa akademi Jaden Philogene na Cameron Archer.

**Tottenham Hotspur**

Mwisho wa msimu uliopita walikuwa watano, wakiwa nyuma ya Man City kwa alama 25. Walianza vema msimu uliopita chini ya Ange Postecoglou na walikuwa nyuma kwa pointi tano kileleni baada ya mechi 10.

Archie Gray, pauni milioni 30 kutoka Leeds, Lucas Bergvall pauni milioni 8.5 kutoka Djurgarden na George Feeney kutoka Glentoran - aliyesajiliwa kwa timu ya vijana chini ya umri wa miaka 18, ndio pekee waliosajiliwa majira ya haya ya joto hadi sasa.

Winga chipukizi wa Korea Kusini, Yang Min-hyuk, atajiunga na kikosi hicho Januari.

Mikey Moore, mshambuliaji wa akademi mwenye umri wa miaka 16, amevutia katika mechi za kirafiki za kabla ya msimu mpya.

Mwandishi wa BBC Sport Nizaar Kinsella anasema: "Kocha Postecoglou ndiye atakayeisukuma Tottenham kushinda taji kwa mara ya kwanza tangu 2008. Hatataka kuweka kikomo katika malengo ya Spurs, lakini kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya litakuwa lengo lao kubwa zaidi."

**Chelsea**

Mwishoni mwa msimu uliopita ilishika nafasi ya sita na alama 28 nyuma ya Man City. Kocha Enzo Maresca, baada ya kuifundisha Leicester na kupanda daraja, alichukua nafasi ya Mauricio Pochettino katika kiti moto cha 'The Blues'.

Wamesajili wachezaji wengi majira ya kiangazi - Kiernan Dewsbury-Hall, Tosin Adarabioyo na Omari Kellyman wote wana uzoefu wa Ligi Kuu England.

Beki mkongwe wa kati Thiago Silva, pamoja na Hakim Ziyech, Ian Maatsen, Lewis Hall na Omari Hutchinson - wote walikuwa nje kwa mkopo msimu uliopita - wameondoka moja kwa moja. Na Conor Gallagher anatarajiwa kuhamia Atletico Madrid.

Mwandishi wa BBC Sport Nizaar Kinsella anasema: "Kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya na kufanikiwa kupata mataji mengine yatakuwa ndio matarajio yao, lakini kuna matumaini kwamba kikosi hiki cha vijana kinaweza kukua na kuleta ushindani katika misimu ijayo."

**Newcastle United**

Mwisho wa msimu uliopita ilishika nafasi ya saba na pointi 31 nyuma ya Man City. Newcastle walifanya vema msimu wa 2022-23 kwa kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini kumaliza katika nafasi ya saba msimu uliopita kulionekana kama kushuka chini.

Sasa Newcastle wanatumaini watambakiza Kocha Eddie Howe, ambaye anapendekezwa kuwa Kocha wa England.

Mwandishi wa Soka wa BBC Sport, Simon Stone anasema: "Nilifadhaika kuhusu Newcastle kwamba wanaelemewa na sheria za kifedha, ikimaanisha kuwa wanalazimika kuuza wachezaji wakati wanataka kununua.

"Habari njema ni Alexander Isak, Bruno Guimaraes na Anthony Gordon wote bado wako kwenye klabu hiyo."

**Manchester United**

Mwisho wa msimu walikuwa nafasi ya nane na pointi 31 nyuma ya Man City. Walimaliza vibaya zaidi tangu ligi ya msimu wa 1989-90, walipomaliza katika nafasi ya nane - ingawa msimu huu wameshinda Kombe la FA.

Kocha Erik ten Hag alitarajiwa kupoteza kibarua chake, lakini United waliamua kubaki na Mholanzi huyo baada ya kukaa kwa kipindi cha miaka miwili klabuni hapo.

Man United wametumia fedha kununu vijana wawili msimu huu - mshambuliaji wa Bologna, Joshua Zirkzee kwa pauni milioni 36.5 na mlinzi wa kati wa Lille, Leny Yoro kwa pauni 52.

Hata hivyo, tayari Yoro amejeruhiwa na huenda akakaa nje ya uwanja kwa miezi mingi. Vilevile, wachezaji kadhaa wameondoka kwa uhamisho wa bure akiwamo mchezaji wa zamani wa Kimataifa wa Ufaransa, Raphael Varane na Anthony Martial.

Mwandishi wa BBC Sport, Simon Stone, anasema: "Erik ten Hag lazima aepuke kufanya vibaya msimu huu kwa sababu hawezi kumudu kumaliza nafasi ya nane tena."

## Nukuu


"Kama mnavyojua, tayari nimepata bahati ya kuona mashabiki wa Anfield kama mtazamaji hapo awali, lakini hii itakuwa ni ladha yangu ya kwanza kama Kocha Mkuu wa Liverpool na ninatazamia kuwaona na kuwasikia! - ninyi nyote, ninafahamu utawapa wachezaji wangu, wafanyakazi wangu na mimi mwenyewe sapoti yako yote kwenda mbele," **Kocha npya wa Liverpool, Arne Slot, akiwaita mashabiki wa timu hiyo kufurika Uwanja wa Anfield, kuelekea mechi za msimu mpya uwanjani hapo.**



"Chelsea imekuwa mpenzi wangu. Kila kombe nililoshinda na klabu hiyo ninalipenda sana. Lakini hili kitaaluma labda ni kubwa zaidi kuliko kitu kingine chochote ambacho nimewahi kufanya," **Kocha wa Timu ya Taifa ya Wanawake ya Marekani, Emma Hayes, baada ya kutwaa Medali ya Dhahabu ya Olimpiki kwenye michuano ya Paris 2024 kwa kuifunga Brazil bao 1-0, ubingwa huo umekuja ikiwa ni siku 84 baada ya kubeba taji la Wanawake la Super League akiwa na Chelsea, aliyoiongoza kwa miaka12.**



"Mikataba ni mizuri lakini inaweza kuvunjwa, kama huna furaha kwa nini uwe hapa? Anapendwa sana na timu kwa tabia yake, lakini kama nilivyosema mara nyingi kwa wachezaji, ikiwa anataka kuondoka na anataka changamoto mpya, ni sawa fikiria anabaki wakati hataki kubaki?," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola, kuhusu sababu Julian Alvarez kutimkia Atletico Madrid.**





Beki wa Yanga, Yao Kouassi (chini), akimchezea madhambi, kiungo mshambuliaji wa Simba, Joshua Mutale, katika mechi ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa na Yanga kushinda bao 1-0 wiki iliyopita. Anayeshuhudia pembeni ni Stephane Aziz Ki. Miamba hiyo itakutana tena Oktoba 19, mwaka huu kwenye Ligi Kuu. **MPIGA PICHA WETU**

# MECHI 6 KALI ZA KUTAZAMWA LIGI KUU 2024/25, HIZI HAPA

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi imetangaza ratiba ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2024/25, itakayoanza Ijumaa.

Mechi itakayokata utepe ni kati ya Pamba Jiji FC itakayokuwa nyumbani, Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza dhidi ya Prisons.

Itakuwa ni mechi ya kwanza kwa Pamba Jiji kwenye Ligi Kuu baada ya miaka 23, tangu iliposhuka daraja 2001, kabla ya kupanda msimu huu.

Kuanzia siku hiyo mashabiki watakuwa wakipata burudani walizozikosa za mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara inayotarajiwa kuwa ngumu na mvuto wa aina yake msimu huu.

Ni ligi inayotarajiwa kuwa na presha kubwa kuanzia kwa mashabiki, viongozi hata kwa wachezaji wenyewe.

Katika makala haya tunakuletea mechi sita za mzunguko wa kwanza ambazo zinatarajiwa kuwa kali na mvuto mkubwa kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo rekodi za nyuma, takwimu na historia ambapo mashabiki hawapaswi kuzikosa kuziangalia laivu uwanjani au kwenye luninga zao.

1. Prisons vs Simba (Oktoba 22)

Moja ya timu ambazo zimeikosesha Simba, si ubingwa tu, bali hata kushiriki Ligi ya Mabingwa Afrika ni Prisons. Kipigo cha mabao 2-1 ilichokipata Machi 6, mwaka huu, katika mchezo wa mzunguko wa pili Ligi Kuu Tanzania Bara, kilionekana kuitoa kabisa kwenye reli inayoelekea katika ubingwa wa Tanzania Bara na kweli ikawa hivyo.

Simba inakwenda kukutana tena na Prisons kwa mara ya kwanza baada ya kipigo kile ilichokipata, Uwanja wa Sokoine, Mbeya, katika Uwanja huo huo, Oktoba 22, mwaka huu, ikiwa ni mchezo wa raundi ya tatu.

Mashabiki watataka kuona Simba hii iliyosheheni wachezaji wengi wapya, ambao wameonyesha tumaini kubwa kwa wanachama na mashabiki wake kama inaweza kukubali tena kipigo kama hicho, au italipiza kisasi na kukumbusha Prisons kuwa yenyewe ni timu kubwa na ukiona Simba ameloa usidhani ni paka.

**2. Yanga vs JKT Tanzania (Oktoba 22)**

Mara ya mwisho zilipokutana zilitoka suluhu katika mchezo ambao Yanga bado ilikuwa na presha ya matokeo ili kuufukuzia ubingwa wa Tanzania Bara. Mechi hiyo ilichezwa Aprili 24, mwaka wakifukuzwa na wapinzani wao, Simba na Azam FC.

Hata hivyo, walilalamikia hali ya uwanja siku hiyo, ambayo ilikuwa ya maji na matope, na ikumbukwe kuwa mechi hiyo ilichezwa siku ya pili, baada ya kushindikana kufanyika Aprili 23.

Timu hizo zinakwenda kukutana katika mechi ya mzunguko wa kwanza, Oktoba 22, mwaka huu, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam. Mashabiki wa soka wana hamu ya kuangalia nini kitatokea tena, ni yale yale au kuna mabadiliko.

**3. Azam vs Simba (raundi ya nne)**

Azam na Simba zitakutana katika mechi ya raundi ya nne ambayo bado haijapangiwa tarehe kutokana na timu hizo kushiriki michuano ya kimataifa.

Kwa sasa nchini, zinapokutana timu hizi zinahesabika kuwa ni moja kati ya mechi kubwa katika Ligi Kuu ya Tanzania Bara.

Mashabiki wa soka nchini watataka kuiangalia mechi hiyo msimu huu hasa ya raundi hiyo ya kwanza ili kupata taswira ya vikosi vya timu hizo mbili.

Timu hizo zimesajili wachezaji kadhaa wapya, hasa Simba ambayo imesajili wengi zaidi, hivyo wanataka kuona kandanda na ufundi uwanjani.

Msimu uliopita, Simba ilivuna pointi nne kwa Azam, zikitoka sare ya bao 1-1, katika Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza, Februari 9, mwaka huu, na kuichakaza kwa mabao 3-0, Mei 9, mwaka huu, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**4. Simba vs Namungo (raundi ya tano)**

Simba itakutana na mfupa mgumu kwake msimu uliopita, Namungo FC, ambayo ilishindwa kuchukua ponti tatu katika mechi zote mbili.

Ni timu ambayo ilikuwa inafifisha matumaini yake ya kuelekea kwenye ubingwa kila inapokutana nayo. Katika mechi ya mzunguko wa kwanza msimu uliopita, zilitoka sare ya mabao 2-2, mechi ikipigwa Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi, Aprili 30, na kutoka sare ya bao 1-1, Novemba 9, mwaka huu, Uwanja wa Azam Complex.

Mechi hiyo itakuwa ya raundi ya nne na bado haijapangiwa tarehe kwa sababu imekaribiana na kalenda ya mechi za kimataifa za Simba inayocheza Kombe la Shirikisho barani Afrika.

**5. Azam vs Coastal (raundi ya tano)**

Ni mechi ambayo Coastal watataka kulipiza kisasi cha kufungwa mabao 5-2 kwenye mchezo wa nusu fainali ya Ngao ya Jamii Alhamisi iliyopita, Uwanja wa New Amaan Zanzibar.

Tarehe kamili ya mechi hii ya mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu haijatajwa kutokana na Coastal kuwa mshiriki wa michezo ya kimataifa, Kombe la Shirikisho barani Afrika, lakini ni mchezo wa raundi ya tano.

Ukiachilia mbali mechi ya Ngao ya Jamii, zinapokutana timu hizo katika ligi panachimbika kweli kweli. Msimu uliopita katika mechi ya mzunguko wa kwanza, Machi 6, zilitoka sare ya bao 1-1, Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, Dar es Salaam, na Azam ikashinda kwa tabu, bao 1-0, Oktoba 6, mwaka huu, Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

**6. Simba vs Yanga (Oktoba 19)**

Wababe wa Ligi ya Tanzania, Simba na Yanga, watakutana Oktoba 19, mwaka huu katika mchezo wa mzunguko wa kwanza.

Ni mechi inayosubiriwa na mashabiki wengi ili kuangalia kama Yanga itaendeleza ubabe tena dhidi ya Simba, baada ya kuifunga mara tatu mfululizo, mara mbili kwenye Ligi Kuu na moja, Ngao ya Jamii, Alhamisi iliyopita.

Aprili 20, Yanga ilishinda mabao 2-1, na Novemba 5, mwaka huu, ikaichakaza mabao 5-1, kabla ya Alhamisi iliyopita kushinda tena bao 1-0, mechi zote zikipigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Wengi wanataka kuona baada ya wachezaji wapya wa Simba kupata mechi za kutosha na muunganiko kama wanaweza kupoteza tena, kutokana na kiwango kikubwa walichokionesha Alhamisi iliyopita katika mechi ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii.

## JE, WAJUA?



HAWA ndio wachezaji bora wa msimu ama wenye thamani zaidi Ligi Kuu Bara (MVP), kwa kipindi cha miaka 10, tangu 2015 hadi 2024; Simon Msuva (2015 - Yanga), Juma Abdul (2016 - Yanga), Mohamed Hussein (2017 - Simba), John Bocco (2018 - Simba), Meddie Kagere (2019 - Simba), Clatous Chama (2020 - Simba), John Bocco (2021- Simba), Bangala (2022 - Yanga), Fiston Mayele (2023 - Yanga), Stephane Aziz Ki (2024 - Yanga).

# Neema wakulima wa pamba, mbolea mpya yabuniwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISA Kilimo wa Bodi ya Pamba Tanzania (TCB), Daniel Bariyanka, amesema wamepata suluhisho la virutubisho vya zao hilo kwa kutengeneza mbolea hai yenye uwezo wa kuwasaidia wakulima kurutubisha mazao yao shambani.

Alisema hayo juzi jijini hapa, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu elimu wanayoendelea kuitoa kwa wakulima juu ya shughuli zinazofanya na bodi hiyo.

"Mbolea hii ni ya maji yenye virutubisho vyote vikuu vitatu, lakini pia yenye virutubisho vidogo vidogo vya aina tano, na tunaposema virutubisho vidogo vidogo na virutubisho vikubwa tunamaanisha kwamba mmea wowote ule hasa mmea wa pamba ili ukue na uzae vizuri unahitaji kupata virutubisho vya aina 17 ambapo kati ya hivyo ndipo vinakuwa virutubisho vidogo na vikubwa," alisema.

Alisema mbolea hai hiyo ni ile ambayo wanaweza kuitengeneza kwa kutumia malighafi yanayopatikana kwa wakulima wenyewe, ikiwamo kutumia kinyesi cha ng'ombe kibichi, majivu, mkaa, chokaa pamoja na kuongeza sukari.

Pia, alitoa wito kwa wakulima baada ya kupata elimu ya matumizi ya mbolea waitumie shambani kwasababu ndiyo suluhisho la virutubisho ambavyo vinapatikana katika mimea ya pamba ili uweze kukua vizuri.

Ofisa Kilimo kutoka Bodi ya Pamba Tanzania, Renatus Filbert, alitoa wito kwa wakulima kufuata kanuni za kilimo bora cha zao hilo kwa kuzingatia kipimo kipya cha upandaji cha sentimita 60 mstari kwa mstari na sentimita 30 mche kwa mche.

Alisema: "Kipimo hiki kimeonesha ufanisi kwa kuongeza uzalishaji wa eneo ambapo zaidi ya asilimia 70 sasa ya wakulima wameweza kufuata hiki kipimo na matokeo yake imeonekana wakulima wengi wameanza kupata mavuno mengi ya kuanzia kilo 1,000 kwa hekari".

# Mradi kuinua wakulima wadogo waanzishwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SHIRIKA la maendeleo lisilo la kiserikali la WE Effect, linatekeleza mradi wa kusaidia kuwainua wakulima wadogo ili waweze kupiga hatua kiuchuni, ikiwamo kuweza kukopeshwa na taasisi za fedha.

Ofisa Mawasiliano wa shirika hilo kutoka Kanda ya Mashariki, Catherine Waking'a alisema mradi huo unatekelezwa ndani ya miaka mitano na utaleta manufaa kwa wakulima wadogo ambao wanakwenda kujiinua kiuchumi.

Waking'a alisema lengo ni kuona wakulima wote wananufaika ikiwamo kukopeshwa na taasisi za fedha ili waweze kupiga hatua katika kilimo cha uzalishaji wanachofanya katika maeneo mbalimbali nchini.

Hata hivyo, alisema We Effect imekuwa ikitoa elimu ya ujasiriamali kwa wakulima, lengo likiwa ni kuwaona wanasonga mbele na siyo kufanya kilimo cha mazoea ambacho hakina tija.

Kadhalika, aliishukuru serikali kutokana na ushirikiano unaotoa

kuhakikisha wanatekeleza miradi yao ya maendeleo ambayo inachangia kuwanuia wakulima wadogo, ili waweze kusonga mbele katika kilimo wanachofanya.

Ofisa wa Benki ya Uchumi Community, Elihuruma Nkini, alisema hivi sasa wanatoa elimu ya utunzaji fedha kwa wajasiriamali ili waweze kufanya maendeleo kupitia mikopo midogo wanayowapa kwa ajili ya uzalishaji.

# Maofisa ugani wapewa tano kuwawezesha wakulima

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imekipongeza Chama cha Maofisa Ugani Tanzania (TSAEE), kwa kuwawezesha wakulima, wafugaji na wavuvi kuzalisha kwa tija na kusaidia nchi kujitosheleza kwa chakula hasa nafaka.

Mratibu wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi kutoka Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Wilson Shimo, alibainisha hayo juzi wakati akifunga kongamano la maofisa ugani nchini lililoandaliwa na TSAEE.

Kongamano hilo liliwakutanisha maofisa ugani kutoka sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi nchi nzima, lengo likiwa ni kujifunza teknolojia mpya kwenye maonesho ya Kilimo Nanenane.

"Nitumie nafasi hii kuwapongeza na kuwashukuru kwa niaba ya serikali kwa kazi nzuri na kubwa mnayoifanya ya kutumia utaalamu wenu kutoa ushauri wa kitaalamu kwa jamii kwenye sekta zote tatu za kilimo, mifugo na uvuvi kuweza kuongeza tija na kupelekea utoshelevu wa chakula katika nchi yetu," alisema.

> **Alisema jukumu la kuwapatia maofisa ugani mafunzo rejea sambamba na vitendea kazi ni la wizara zote za kisekta kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI.**

Aliongeza: "Hususani katika kilimo cha nafaka na ndiyo maana serikali inaendelea kuboresha mazingira yenu ya kazi ili mfanye kazi vizuri zaidi". Alisema kwa kutambua mchango wao na kuboresha mazingira ya utoaji huduma serikali imenunua magari 15, pikipiki kwa maofisa ugani nchi nzima, vishikwambi 4,305, vifaa vya kupima udongo na ujenzi wa nyumba 50 za maofisa ugani kwenye ngazi za kata unaendelea.

Alisema jukumu la kuwapatia maofisa ugani mafunzo rejea sambamba na vitendea kazi ni la wizara zote za kisekta kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais TAMISEMI.

Aidha, alisema hadi sasa Tanzania kuna maofisa kilimo ugani 7,000 kwa upande wa kilimo, mifugo (3,642) na uvuvi (647) na kwa takwimu hizo inaonesha kuwa idadi hiyo bado ni ndogo ikilinganishwa na maeneo yaliyopo.

Alisema zipo kata 3,659, vijiji 12,319, mitaa 4,233 na haya yote yanahitaji kuwa na maofisa ugani lakini pamoja na uchache wao bado wanatoa huduma nzuri kukidhi mahitaji.

Mwenyekiti wa Chama cha Wagani Tanzania (TSAEE) Prof. Catherine Msuya kutoka Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA) alisema chama hicho kimeanzishwa mahususi kwa lengo la kuwakutanisha wagani kwa pamoja.

Alisema pia kubadilishana uzoefu na kubuni mbinu za pamoja za kusaidia utoaji huduma kwa jamii ili kusaidia kuongeza tija na kuinua uchumi wa Taifa.

Kadhalika, alisema mwaka huu wamekutana kwenye wakati wa maonesho ya Nanenane jijini Dodoma ili kujifunza teknolojia na mbinu mbalimbali.




Rais Samia Suluhu Hassan akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Azania Bank, Esther Mang'enya, alipotembelea banda la benki hiyo kwenye maonesho ya Nanenane jijini Dodoma wiki iliyopita. Azania Bank ilikuwa mdhamini mkuu wa maonesho hayo yaliyohitimishwa wakati wa kilele cha Sikukuu ya Wakulima Agosti 8. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ujenzi zahanati waleta ukombozi wakazi Mkalama

**Na Thobias Mwanakatwe,** MKALAMA

WANANCHI wa vijiji vya Igonia na Kinakamba Wilaya ya Mkalama mkoani Singida wameishukuru serikali kwa kuwasogezea huduma za afya karibu.

Wamesema hatua hiyo itawasaidia kupunguza adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

Walitoa shukrani hizo juzi wakati wa uzinduzi wa Zahanati ya Kijiji cha Kinakamba iliyopo Kata ya Ibaga pamoja na Zahanati ya Kijiji cha Igonia iliyopo Kata ya Ibaga wilayani Mkalama.

Mkazi wa Kijiji cha Igonia, Elipendo Samweli, alisema kwa muda mrefu wamekuwa wakitembea umbali mrefu kufuata huduma hizo katika vijiji vya Mkalama, Gumanga na Nduguti.

"Tunaishuruku sana serikali, hatukuwahi kuwa na zahanati katika kijiji chetu. Leo hii mimi kama mama, zahanati hii itasaidia kupata huduma mbalimbali kama vile watoto kupata chanjo kwa wakati, wajawazito kufika kliniki kwa wakati, " alisema.

Naye Rajabu Issa Mkumbo, mkazi wa Kijiji cha Kinakamba alisema kufunguliwa kwa zahanati hiyo itawasadia kuondoa gharama za kusafiri kufuata huduma hizo katika vijiji vya Mkalama, Nduguti pamoja na Gumanga.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, James Mkwega akizungumza wakati wa uzinduzi wa zahanati hizo amewataka wananchi hao kutoa ushirikiano kwa watoa huduma watakaoletwa na serikali pamoja na kuwaomba kuchangia damu.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Dk. Solomon Michael aliwataka watumishi wa afya kutoa huduma bora, kuwasisitiza wananchi kujiunga na Bima ya Afya ya CHF.





# Upotevu magunia 200 ya kakao

## -RC atoa siku 30 kurejeshwa

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

SAKATA la upotevu wa magunia zaidi ya 200 ya kakao za wakulima wilayani Kyela, limechukua sura mpya baada ya kampuni inayosimamia maghala kupewa siku 30 kurejesha magunia hayo, ama kulipa fedha zenye thamani ya magunia hayo.

Uamuzi huo ulifikiwa juzi wakati wa kikao cha viongozi wa Vyama vya Msingi vya Wakulima wa Kakao (AMCOS) na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mbeya kilichokuwa na lengo la kujadiliana namna ya kutatua tatizo hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alisema kwenye mnada namba tatu wa Julai 15, mwaka huu kulikuwa na magunia 1,915 ambayo yalikuwa yanauzwa na baada ya mnada kukamilika magunia 200 yalipotea katika mazingira ya kutatanisha.

Alisema magunia hayo yaliyopotea yalikuwa na thamani ya Sh. milioni 440 na hivyo kuhatarisha uchumi wa wakulima waliokuwa wamepeleka magunia hayo kuuzwa.

Alisema baada ya tatizo hilo kutokea waliwakamata viongozi wa Chama Kikuu cha Wakulima wa Kakao wilayani humo (KYECU) pamoja na baadhi ya wasimamizi wa maghala.

"Mpaka sasa magunia 30 yameshapatikana kwa hiyo naagiza haya magunia yaliyobaki yarejeshwe ndani ya siku 30 na zaidi ya hapo tutachukua hatua kali zaidi," alisema Homera.

Hata hivyo, Kampuni ya Ngonde Traders ambayo inatuhumiwa kusababisha upotevu wa magunia hayo iliomba iongezwe muda wa kurejesha magunia hayo ikiomba kupewa miezi mitatu badala ya mwezi mmoja.

Mwakilishi wa kampuni hiyo ambaye alijitambulisha kwa jina moja la Rehema, alisema wakipewa miezi mitatu watakuwa na muda wa kutosha kutangaza mali walizonazo ili ziuzwe na kupata fedha za kulipa deni hilo.

"Kimsingi sisi hatujachukua fedha lakini tunapambana kama kampuni ili kuhakikisha tunalipa fedha ili kulinda heshima tuliyonayo, tunaomba mtuombee!," alisema Rehema.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Josephine Manase, alisema kutokana na sakata hilo wakulima walikuwa wameanza kupanga kuandamana ili kushinikiza walipwe fedha zao jambo ambalo alisema lilikuwa linatishia hali ya utulivu.

Alisema baadhi yao walikuwa wameanza kwenda ofsini kwake kulalamika lakini kwa kushirikiana na viongozi wa AMCOS walifanikiwa kuwatuliza waache.

Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Stakabadhi za Ghala (WRRB), Asangye Bangu aliwatahadharisha viongozi wa vyama vya ushirika kuepuka kufanya vitendo ambavyo havina tija kwa wakulima akidai kuwa watawashughulikia. Vilevile aliwataka wasimamizi wa maghala kutowazuia mameneja wa vyama vya ushirika kukagua magunia ya wakulima yaliyohifadhiwa kwenye maghala yao.

Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Mbeya, Maghela Ndimbo, alisema mpaka sasa wanawashikilia baadhi ya viongozi wa Kampuni ya Ngonde Traders kwa ajili ya mahojiano.




Katibu Mkuu Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Xavier Daudi, akizungumza katika Mkutano Mkuu wa kwanza wa Mfuko wa Uwekezaji Faida uliofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF ambaye alikuwa Mwenyekiti wa Mkutano huo, Abdul-Razak Badru na Mwakilishi wa Benki ya CRDB ambao ni wasimamizi ma waangalizi wa fedha za uwekezaji, Ahmed Masumai. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtaji Benki ya Mwanga Hakika wafikia Bil.25/-

**Na Mwandishi Wetu**

MTAJI wa hisa katika Benki ya Mwanga Hakika umekua kutoka Sh.bilioni 17.11 mwaka 2023 hadi Sh. bilioni 25.36 mwaka huu, ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni 8.3.

Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Jagjit Singh, alieleza hayo juzi wakati wa mkutano mkuu wa nne wa wanahisa wa benki hiyo.

Singh alisema benki hiyo imeandaa mpango mikakati mpya kwa mwaka 2021-hadi 2025 ikiweka msisitizo kuboresha huduma kwa wateja na kupanua wigo wa kibiashara ili iweze kuwa shindani ndani na nje ya Tanzania.

Alisema kwa kipindi cha mwaka 2023 benki hiyo imewekeza katika mfumo mkuu wa kibenki pamoja na vifaa vya kuhifadhia mifumo ya kibenki, malipo ya kiserikali, mfumo wa NIDA na mikopo ya kidijitali.

"Benki inaendelea kuweka msisitizo katika kuboresha huduma zake ili ziwe za kisasa zaidi na kuongeza ubora wa huduma za TEHAMA na kidijitali ili wateja wengi zaidi waweze kufikiwa na kupata huduma zetu popote walipo," alisema.

Alisema kwa mwaka 2024 benki imeendelea kuimarisha mtaji wake kupitia faida na kuweza kufanya biashara zaidi na kuendelea kukidhi vigezo vya Benki Kuu.

Alisema kufikia Juni 2024 mtaji wa benki wa kisheria ulikuwa Sh. bilioni 37.40 juu ya ukomo wa chini wa Benki Kuu wa mtaji wa benki ya kibiashara Sh. bilioni 15.

Aidha, alisema kwa mwaka 2024 benki hiyo ilikusudia kuongeza amana za benki zilizokuwapo Desemba 2023 Sh. bilioni 142.19 mpaka kufikia Sh. bilioni 172.36, ambapo alisema mpaka kufikia mwishoni mwa Juni, 2024 amana za benki zimefikia Sh.bilioni 180.76.

Alisema: "Mwaka 2024 mikopo imekadiriwa kuongezeka mpaka kufikia Sh.bilioni 167.44 kutoka Sh.bilioni 131.44 mwaka 2023, hivyo hadi kufikia Juni, mwaka huu mikopo imefikia kiasi cha Sh. bilioni 171.96".

Alisema faida kabla ya kodi imeongezeka na kufikia Sh. bilioni 14.99 na hivyo mpaka kufikia Juni mwaka 2024 faida kabla ya kodi imefika Sh.bilioni 7.54.

Mwenyekiti wa bodi hiyo, Ridhuan Mringo alisema benki hiyo imeendelea kuimarika na kufanya vizuri kwa mwaka 2023 katika nyanja mbalimbali za kifedha.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa benki hiyo, Raymond Tarimo, alisema benki hiyo imejipanga kukabiliana na changamoto zijazo za kiteknolojia.

Hivyo, alisema imeanzisha Kituo cha Mafunzo cha Mwanga Hakika Training Academy ambacho kimekuwa kikifundisha vijana fani mbalimbali za kibenki hususani kwenye masuala ya fedha na teknolojia.

Alisema: "Sisi kama benki tulianzisha hili mwaka jana na tumepata vijana waliohitimu mara ya kwanza, vijana hawa tayari wanasambazwa kwenye matawi yetu na wengine makao makuu kwa ajili ya kuandaa vijana kukabiliana na mazingira ya kibenki yaliyoko sasa na baadaye."

# Waandishi wa habari wakumbushwa wajibu wao

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

WAANDISHI wa habari mkoani hapa wametakiwa kuandika habari zitakazosaidia kutatua kero za wananchi kwa maelezo kuwa habari hizo zitasaidia kurejesha imani ya wananchi kwa vyombo vya habari.

Mkurugenzi wa Umoja wa Klabu za Waandishi wa Habari nchini (UTPC), Keneth Simbaya, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na waandishi wa habari wa Mkoa wa Mbeya alipokuwa kwenye ziara ya kikazi mkoani humo.

Simbaya alisema kwa miaka ya karibuni imani ya wananchi kwenye vyombo vya habari imeshuka kutokana na waandishi wa habari kuripoti habari ambazo hazina tija kwao.

Alizitaka klabu za waandishi wa habari kutumia vyombo vyake zikiwamo televisheni za mtandaoni kuandika habari za wananchi kwa madai kuwa kwa sasa imani ya wananchi imebaki kwenye klabu hizo.

"Nawaomba sana waandishi wa habari tuandike habari ambazo zinaigusa jamii moja kwa moja, wananchi wanataka habari ambazo zinatatua kero zao, wananchi wanahitaji habari ambazo zinatatua kero za maji, barabara na shida zao zingine," alisema Simbaya.

Hata hivyo alisema Chama cha Waandishi wa Habari Mkoa wa Mbeya (MBPC) ni miongoni mwa vyama ambavyo vina maendeleo mazuri ikiwamo uendeshaji wa kikundi cha kuweka na kukopa (VICOBA) na kuwa mfano kwa nchi nzima.

Aliwataka viongozi wa MBPC kuendelea kuwaunganisha waandishi wa habari wa mkoa huo ili kuwa na nguvu zaidi akidai kuwa vyama vya waandishi wa habari vya mikoa vikiwa imara vinasababisha hata UTPC kuwa imara zaidi.

Mwenyekiti wa MBPC, Nebart Msokwa alisema mpaka sasa chama hicho kina wanachama 70 awanne ambao ni wanachama wa heshima.

Alisema kati ya wanachama hao, 40 wamejiunga kwenye VICOBA ambavyo ni moja kati ya njia za kuwainua wanahabari kiuchumi na kuondokana na tatizo la umaskini ambalo limekuwa likiwakabili.

"Kupitia VICOBA wanachama wanakopeshana fedha ambazo wanazitumia kwa ajili ya kufanya shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwamo ujenzi wa nyuma, kusomesha watoto na hata kuanzisha biashara," alisema Msokwa.

Mwenyekiti wa Mbeya Press VICOBA, Ezekiel Kamanga, alisema mpaka sasa chama hicho kina zaidi ya Sh. milioni 38 ambazo ni hisa za wanachama na kwamba mzunguko wa mikopo ni zaidi ya Sh. milioni 58.



## Dk. Mwinyi kufungua Tamasha Kizimkazi, Samia kufunga

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

TAMASHA la Kizimkazi limetangaza wadhamini wa tamasha hilo ambalo linatarajiwa kuzinduliwa Agosti 18, mwaka huu na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi na kufungwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Agosti 25.

Mwenyekiti wa kamati wa tamasha hilo, Mahfoudh Said Omar, alisema maandalizi ya tamasha hilo yamefikia pazuri na la mwaka huu ni la aina yake kuliko yaliopita.

Aliwataka wadhamini hao kuwa ni taasisi za kibenki ikiwamo NBC, CRDB, NMB, PBZ, TADB, Kampuni ya Simu ya TTCL, Tigo-Zantel, Taasisi ya Wanawake Initiative, Bodi ya Watalii Tanzania (TTB), Kamisheni ya Utalii Zanzibar na NSSF.

Alisema tamasha hilo litahusisha shughuli mbalimbali za kimaendeleo, kiuchumi na kiutamaduni, kutakua na uzinduzi wa miradi ya maendeleo ikiwamo ufunguzi wa Shule ya Tasani Makunduchi na jengo la afya la huduma ya afya ya mama na mtoto huko Kizimkazi.

Makamu Mwenyekiti wa kamati ya tamasha hilo, Mustafa Muhamed Haji, alisema ni mwaka wa tisa kuanza tamasha hilo ambalo limeleta maendeleo katika Kijiji cha Kizimkazi.

Alisema tamasha la mwaka huu litafungua fursa za kiuchumi na kimaendeleo ambapo Kizimkazi ya sasa ni tofauti na ya miaka tisa iliyopita.

Alisema hivi sasa Kizimkazi ina hospitali ya kisasa kwa ajili ya huduma za afya ya mama na mtoto, ambapo awali wananchi wa kijiji hicho walikuwa wakitembea umbali mrefu kufuata huduma hiyo.

# NMB kukabidhi skuli kwa Rais Samia

Na Mwandishi Wetu,
ZANZIBAR

KAMATI ya Maandalizi ya Tamasha la Kizimkazi (Kizimkazi Festival 2024) imetambulisha rasmi wadhamini wa mwaka huu, ikiwamo Benki ya NMB, ambayo pamoja na mambo mengine, itanoa wajasiriamali zaidi ya 700 na kukabidhi Skuli ya Maandalizi ya Tasani iliyoko Makunduchi, Zanzibar.

Kizimkazi Festival ni tamasha linalotumika kuzindua miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) na wadau wa maendeleo, zikiwamo taasisi binafsi, ambalo mwaka huu litazinduliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi Agosti 18.

Akizungumza wakati wa utambulisho wa wadhamini hao, Meneja wa Biashara wa NMB Zanzibar, Naima Said Shaame, alisema benki yake itashiriki kwa ukubwa tamasha hilo kuanzia leo Agosti 12 hadi siku ya uzinduzi na hatimaye kufungwa kwa tamasha hilo Agosti 25.

Alibainisha ya kwamba katika tamasha hilo kwa mwaka 2024, Benki ya NMB itafanya mambo makuu matatu yakijumuisha mafunzo kwa wajasiriamali zaidi ya 700, ambao watakuwa wakipewa elimu ya fedha, uwekezaji na uimarishaji wa shughuli zao za kijasirimali.

"Pili, kutakuwa na siku maalum iitwayo NMB Day, ambayo itakuwa Agosti 20, siku hiyo kutakuwa na matukio matatu, ambayo ni uzinduzi na kukabidhi Skuli ya Maandalizi ya Tasani, ambayo itakabidhiwa kwa Rais Samia, ambaye ndiye aliyeweka jiwe la msingi Agosti 29, mwaka jana," alisema.

**"Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zinakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi na wananchi tunakata miti sana na hatuna utamaduni wa kupanda miti kwa wingi," alisema.**

Skuli ya Maandalisi ya Tasani iliyoko katika eneo la mita za mraba 467, inajumuisha vyumba vitano vya madarasa yatakayochukua wanafunzi 200, sawa na wanafunzi 40 kila kimoja, ofisi ya mwalimu mkuu, ofisi ya walimu, wafanyakazi, stoo, mifumo ya kisasa ya majisafi na majitaka pamoja na sehemu ya michezo.

"Ukiondoa kukabidhi na kuzindua skuli hiyo, mchana wa NMB Day kutakuwa na michezo kwenye Uwanja wa Dimani, na kisha usiku wake kutakuwa na Usiku wa Singeli kwa ajili ya kuwafungulia fursa wasanii wa aina hiyo ya muziki walioko visiwani Zanzibar.

"Jambo la tatu litakalofanywa na NMB katika Kizimkazi Festival 2024, kuwapo banda la benki yetu katika viwanja vya maonesho, ambalo pamoja na mambo mengine, litatoa huduma za kifedha, elimu ya fedha, taarifa mbalimbali za kibenki kwa wananchi watakaohudhuria kwa siku zote za tamasha," alisema Naima.

Akitambulisha wadhamini wa tamasha hilo, Mwenyekiti wa Tamasha la Kizimkazi, Mahfudh Said Omar, alitaja wadhamini wenza wa Kizimkazi Festival 2024, mbali na NMB, ni pamoja na Bodi ya Utalii Tanzania, Mwanamke Initiatives Foundation, ASAS, CRDB, NBC, TADB, PBZ, TIB, Infocus Studio, Livestream, DSFA, TAHA, BoT, Tallahassee Community College na Tanzania Unforgettable.




Wananchi waliojitokeza katika Viwanja vya Mnazi Mmoja wakipanga mstari kwa ajili ya kupata huduma za bure zilizotolewa katika kambi ya siku tatu jijini Dar es Salaam iliyoandaliwa na Jumuiya ya Khoja Shia Ithnaashari katika kuenzi kifo cha Mjukuu wa Mtume Muhammad (S.A.W), Imamu Hussein miaka 1,400 iliyopita katika Kalbar nchini Iraq. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ripoti: Wananchi wanaogopa kutumia gesi kupikia

Na Rahma Suleiman,
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA, Zanzibar), Dk. Mzuri Issa, amesema bado elimu ya matumizi ya nishati mbadala inahitajika kwa sababu baadhi ya wananchi wanaogopa kutumia nishati hiyo kupikia.

Alisema hayo kwenye kikao cha uwasilishwaji wa ripoti ya tathmini ya jinsi vyombo vya habari Zanzibar vinavyoripoti habari za wanawake na uongozi katika mabadiliko ya tabianchi na uhimilivu.

Alisema wanawake ndiyo waathirika zaidi wa athari za mabadiliko ya tabianchi kutokana na kutumia nishati ya kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia, hivyo elimu hiyo ya matumizi ya nishati mbadala itasaidia kuepukana na changamoto mbalimbali ikiwamo za kiafya.

Hivyo, aliwataka waandishi wa habari kufanya utetezi kwa wananchi hasa pale wanapoona kuwa kuna mambo hayapo sawa na kuhakikisha usawa wa kijamii unapatikana.

Alisema hivi karibuni Tanzania kumezinduliwa mkakati wa kitaifa wa kupambana na mabadiliko ya tabianchi, jambo ambalo ni zuri kwa sababu (Tanzania) ni moja ya nchi ambayo haifanyi vizuri katika hilo na matumizi ya misitu ni makubwa.

"Tanzania ni miongoni mwa nchi ambazo zinakabiliwa na athari za mabadiliko ya tabianchi na wananchi tunakata miti sana na hatuna utamaduni wa kupanda miti kwa wingi," alisema.

Alisema Tanzania imeridhia matamko mbalimbali ya kufikia usawa wa kijinsia duniani, hivyo lazima kufanya jitihada za kufikia asilimia 50 kwa 50 na kwa kila sekta kuhakikisha kuna sauti za wanaume na wanawake, ikiwamo kwenye mabadiliko ya tabianchi.

Mkurugenzi wa Community Forest Pemba (CFP), Mbarouk Omar Mussa, aliwataka waandishi wa habari kuwa mabalozi wazuri katika kuelimisha umma kuhusu athari za mabadiliko ya tabianchi.

Pia aliwataka waandishi wa habari kujikita katika uandishi wa habari za mazingira ili kupunguza athari za kimazingira zinazotokana na mabadiliko ya tabianchi.

Akitoa muhtasari wa ripoti ya tathmini ya jinsi vyombo vya habari Zanzibar vinavyoripoti habari za wanawake na uongozi katika mabadiliko ya tabianchi na uhimilivu, Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Zanzibar (SUZA), Dk. Salum Suleiman Ali, alisema katika magazeti manne waliyopitia taarifa zao kutoka Januari hadi Mei mwaka huu Nipashe linaongoza kuandika habari nyingi zinazohusu mabadiliko ya tabianchi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**DAUD VICTOR NTAYEGA** atangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S1351-0563** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **BURONGE SECONDARY SCHOOL** mwaka 2021. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/UBU/166320/2024**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**HAMISI MAHMOUD MATUNGULU** anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria namba **TAE062215** iliyotolewa uhamiaji makao makuu Dar es salaam .kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/166722/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**RUZNA SEIF NYINGIA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S 1741-0182** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **CHAMAZI DAY SECONDARY SCHOOL** mwaka **2022**. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/TEM/160606/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**FLORAH ANNA MNKANDE** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ZANAKI SECONDARY SCHOOL** mwaka **1980.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI CONTROL NUMBER : 9910841949971**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EDINA VERONICA SABAS** anatangaza kupotea kwa **CHETI CHA KIDATO CHA NNE** chenye index namba **S 1426-0012** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **SHULE YA SEKONDARI BUJORA** mwaka **2011.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: NJ/RB/2157/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ANNA YACOB MANAWA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne index No **S.5174-0004,2016** Shule ya Sekondari ST.CATHERINE na Kidato cha Sita Index **NO.S0325-0574** Shule ya Sekondari LUGALO, vilivyotolewa na Baraza la mitihani la Taifa Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa polisi: **PHQ/ DOD/DOD/5572/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EZEKIEL MAGOLYO MAIGE** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T 222 BRA.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:**
**PHQ/SHI/KAH/6565/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**AUGUSTINO BAHATI NGENZI** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE USAJILI **MC182 DZH,** CHASSIS NAMBA **LC6PCJK29P0049049** KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE. POLISI TAARIFA: **PHQ/IRI/IRI/11925/2024**.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MATILDA HENRY MTENGA,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya Toyota spacio ,yenye namba za usajili **T766CEE,** CHASSIS NO **AE1116155678,** ENGINE NO 4AH87419, Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **PHQ/DOD/DOD/34134/2024**

## TANGAZO

Mimi **GEDIOSE RWEYEMAMU** namtafuta rafiki yangu Ndugu **SAMWEL MATABA** ambaye nimepotezana naye siku nyingi . Popote alipo tuwasiiane kupitia namba **0692945649 au Email gediose@hotmail.com**

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 11682/ 2024**
**In the matter of the Estate of the late ELIZABETH ROBERT MZAVA of Msalato Within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY JANUARY ALEXANDER MABODO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 12 Day of 8, 2024
Presented for filling this 15 Day of 7, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. 17524/ 2024**
**In the matter of the Estate of the late ANDREW VITALIS CHAKILA of SULUNGAI Within Dodoma Region.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY NHAMBI ANDEW CHAKILA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 Probate Rules Gn. 369 of 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 20th Day of 8, 2024
Presented for filling this 25 Day of 7, 2024.

RESIDENT MAGISTRATE

---

**FORM 58**
**GENERAL CITATION**
**Rule 75**
**IN THE COURT DISTRICT DELEGATE OF ARUSHA DISTRICT**
**AT ARUSHA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 18840 OF 2024**
**In the Matter of the Estate of the Late**
**And**
**In the Matter of Application for Probate of the Will of the Late ( MARRY ABDALLAH SALEWA) BY JOHN LAZARO WENGAS**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they thick fit before the grant of probate is made to the above –named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 19th day of AUGUST 2024 @09:00am By **hon.A.R Ndossy (SRM).**
The Will of the said deceased is deposited and open for inspection at the court .
Date at 09th this day of AUGUST 2024

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/63)**

Mahakama ya Mwanzo ya **ARUSHA MJINI**
Wilaya ya **ARUSHA**
**MADAI NAMBARI 126 ya 2024**
**Mdai VIVIAN APOLINARY SOKA**

Mdaiwa **WAZIRI RAMADHANI MDEE**
Kwa **WAZIRI RAMADHANI MDEE MOSHI .0688 800 225**

Kwa kuwa mdai/ wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba ( Eleza hapa habari za Madai):-

**FIKA HAPA BILA KUKOSA ILI KUJIBU MADAI YA TALAKA**
Kwa hiyo unahitajiwa /mnahitajiwa kuhudhuria Mahakama hii siku ya JUMATATU tarehe **26/08/2024** saa **2:30** asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angali a kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii, itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/ mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakam a hii leo tarehe **9/08/2024**

.........................................
Hakimu /Hakimu Mkazi Mahakama ya Mwanzo

---

**FORM 58**
**IN THE DISTRICT COURT OF TEMEKE**
**AT ONE STOP CENTRE**
**PROBATE AND ADNISTRATION CAUSE NO . 18102 OF 2024**
**In the Matter of the Estate of the Late**
**JOHN MWINAMO**
and
In the Matter of Application for letters of administration by **LAWRENCE JOHN LYAYUKA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule75 )**
All persons claiming to have any interest in the state of the above-named deceased are hereby cited to come and se e the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 19th day of August 2024.

Dated at DAR ES SALAAM this 30th day of July 2024

Principal Resident Magistrate

---

## TANGAZO

Mimi **GEDIOSE RWEYEMAMU** namtafuta rafiki yangu Ndugu **AVELINE SANINI NJAU** ambaye nimepotezana naye siku nyingi . Popote alipo tuwasiiane kupitia namba **0692945649 au Email gediose@hotmail.com**

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701 AU TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Mataifa yalaani Israel kushambulia shule

**GAZA,** PALESTINA

MATAIFA mbalimbali yakiongozwa na mtaalamu huru wa haki za binadamu aliyeteuliwa na Umoja wa Mataifa (UN) Francesca Albanese, ameishutumu Israel kwa kufanya mauaji ya halaiki katika vita vyake huko Gaza baada ya kuilenga shule katika ukanda huo na kuua watu 100.

Albanese, ambaye ni mjumbe maalum anayehusika na masuala ya haki za binadamu katika maeneo ya Palestina alisema jana kuwa Israel inawaua Wapalestina kitongoji kimoja baada ya kingine, kwenye hospitali, shule, kambi za wakimbizi na hata maeneo yanayotajwa kuwa salama.

Katika mtandao wake wa X (zamani Twitter), Albanese alisema Israel imekuwa ikifanya mashambulizi hayo dhidi ya Wapalestina kwa kutumia silaha ilizopewa na Marekani na Ulaya huku akiomba Wapalestina wawasamehe kwa kushindwa kwao kwa pamoja kuwalinda.

Katika ripoti iliyotolewa Machi, Albanese alisema kulikuwa na taarifa za kuridhisha ya kwamba Israel ilifanya vitendo kadhaa vya mauaji ya halaiki katika vita vyake huko Gaza. Huku taifa hilo likimkosoa mpigania haki huyo kwamba anaugeuza ukweli.

Albanese alisisitiza kwamba bila shaka alilaani pia mashambulizi ya Oktoba 7 ya Hamas dhidi ya Israel ambayo yalianzisha vita vya miezi 11 katika Ukanda wa Gaza.

Mkuu wa sera za kigeni wa Umoja wa Ulaya, Josep Borrell, alielezea kusikitishwa na shambulizi hilo baya la Israel dhidi ya shule inayohifadhi watu waliokimbia makazi yao huko Gaza.

Borrell aliandika kwenye mtandao wa X: "Nimeshtushwa na picha za shule hiyo huko Gaza iliyokumbwa na shambulizi la Israel, na inasemekana kuwa makumi ya waathirika wa Kipalestina wameuawa. Angalau shule 10 zililengwa katika wiki zilizopita. Hakuna uhalali wa mauaji haya."

Wizara ya Mambo ya Nje ya Misri ililaani shambulizi hilo na kusema mauaji ya raia wa Gaza yanaonyesha kuwa Israel haikuwa na nia ya kusitisha vita.

Pia ilisema tukio hilo inadhihirisha ni kwa namna gani sheria za kimataifa zinapuuzwa na kwamba shambulio hilo lilikuwa ni mwendelezo wa uhalifu wa kiwango kikubwa dhidi ya idadi kubwa ya raia wasio na silaha.

Utawala wa Hamas ulieleza kuwa watu kadhaa pia walijeruhiwa katika shambulizi hilo, na kwamba Jeshi la Israel lilidai kuwa lililenga kituo cha kamandi cha wanamgambo hao wa Kipalestina.

Aidha, ilielezwa kuwa Misri, Marekani na Qatar wamepanga awamu mpya ya mazungumzo ya kusitisha mapigano siku ya Alhamisi, wakati hofu ikiongezeka ya kutokea mzozo mkubwa zaidi wa kikanda, utakaozihusisha Iran na Lebanon.

Saudi Arabia ilipongeza hatua ya mataifa hayo matatu wapatanishi ya kuzialika Israel na Hamas kurejea kwenye mazungumzo ya kusitisha mapigano ambayo yanatarajiwa kufanyika Agosti 15, mwaka huu.

Hata hivyo, taifa hilo lilithibitisha msaada wake kamili kwa jopo hilo ili kushughulikia kwa haraka kuzorota kwa hali ya kibinadamu huko Gaza.

Uturuki pia ilisema shambulio hilo dhidi ya shule huko Gaza ni uhalifu mpya dhidi ya ubinadamu uliofanywa na Israel na kusababisha vifo vya raia waliokuwa wamekimbilia kwenye shule hiyo.

Serikali ya Ankara ilimtuhumu pia Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu kwa kuhujumu mchakato wa mazungumzo ya usitishwaji mapigano Gaza.

Wakati vita vikiendelea katika Ukanda wa Gaza, Wizara ya Afya eneo hilo inayosimamiwa na Hamas ilisema hadi sasa idadi ya vifo imefikia watu 39,790 tangu kuanza kwa vita hivyo.

***DW, Reuters, AFP***



Wapalestina wakiangalia uharibifu na maafa yaliyosababishwa na shambulio la Israel katika shule huko Gaza. **PICHA: MTANDAO**

# Hezbollah yajibu mashambulizi ya Israel

**BEIRUT,** LEBANON

KUNDI la Hezbollah limesema limerusha ndege zisizo na rubani zilizokuwa na vilipuzi kwenye kambi ya kijeshi kaskazini mwa Israel kujibu mauaji ya kiongozi wa kundi la Hamas yaliyofanyika Lebanon.

Shambulizi la Israel lilimlenga ofisa wa usalama wa Hamas kutoka kambi ya wakimbizi ya Wapalestina ya Ain el-Heloue, alipokuwa kwenye gari lake huko Saida, mji jirani na kambi hiyo. Hamas ilisema kamanda wake Samer al-Hajj aliuawa.

Kundi hilo lilisema lilitekeleza shambulizi hilo Agosti 10, mwaka huu huko Galilaya, na kwamba ni mashambulizi makubwa zaidi tangu kuanza kwa mapigano na jeshi la Israel miezi 10 iliyopita.

Ilielezwa kuwa operesheni hiyo ililenga kambi ya kijeshi yenye maghala ya risasi na vifaa vya usaidizi kusini mwa mji wa Safad huko Upper Galilaya, kilomita 18 kutoka mpakani.

Kwa mujibu wa taarifa ya Hezbollah, ilizindua vikosi kadhaa vya ndege zisizo na rubani zilizojaa vilipuzi kwenye kambi hiyo iliyolengwa kwa mara ya kwanza tangu Oktoba 7.

Pia ilielezwa kuwa chama cha Hassan Nasrallah kilifanya mashambulizi mengine mawili ya ndege zisizo na rubani dhidi ya vituo vya kijeshi vilivyo karibu na mpaka.

Hezbollah pia ilishambulia maeneo mengine saba kuanzia Bahari ya Mediterania hadi miinuko ya Golan, iliyokaliwa kwa mabavu na Israel.

Kutokana na jibu la Hezbollah, jeshi la Israel, kwa upande wake, lilianzisha mashambulizi ya anga na kushambulia maeneo kumi na tano ya kusini mwa Lebanon kwa mizinga.

Ndege za Israel pia zilivunja kizuizi cha sauti juu ya mji wa Beirut na vitongoji vyake vya kusini, na kusababisha milipuko yenye nguvu ambayo ilizua hofu miongoni mwa watu.

***RFI***

## Marathon ya CRDB yakusanya Faranga milioni 120 kusaidia waathirika mafuriko

**BUJUMBURA,** BURUNDI

MARATHON ya Benki ya CRDB imeandika historia nyingine baada ya kufanyika kwa mara ya pili nje ya mipaka ya Tanzania, ikifanyika katika Jiji la Bujumbura na kuvutia zaidi ya washiriki 1,500.

Kwa pamoja, washiriki hao wamefanikisha lengo kuu la kukusanya Faranga za Burundi milioni 120 kwa ajili ya kusaidia waathirika wa mafuriko yaliyokumba eneo la Ziwa Tanganyika mapema mwaka huu.

Waziri wa Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Vijana, Michezo na Utamaduni wa Burundi, Gervais Abayeho, alikuwa mgeni rasmi katika tukio hilo la kihistoria, akiambatana na Meya wa Jiji la Bujumbura, Jimmy Hatungimana na viongozi wengine wa Serikali ya Burundi.

Balozi wa Tanzania Burundi, Gelasius Byakanwa, pia alihudhuria pamoja na viongozi waandamizi wa Benki ya CRDB wakiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya CRDB Bank Burundi, Hosea Kashimba na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Bruce Mwile.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mbio hizo zilizobeba kaulimbiu ya "Tabasamu Limevuka Mipaka," Waziri Abayeho alipongeza Benki ya CRDB kwa kuwaleta pamoja watu wa Burundi na mataifa jirani kwa lengo la kusaidia waathirika wa mafuriko.

"Kujitoa kwenu ni mfano mzuri kwetu sote. Ushirikiano huu unaonesha ni kwa jinsi gani tunavyoweza kufanikisha mambo makubwa tunapokuwa na mshikamano. Hongereni Benki ya CRDB na CRDB Bank Foundation kwa jitihada zenu za kusaidia wenzetu walioathirika," alipongeza Abayeho.

Waziri huyo alisisitiza kuwa mbio hizi zinahusiana moja kwa moja na Dira ya 2040-2060 ya Burundi, ambayo inalenga kuifanya nchi hiyo kuwa na amani, uchumi shindani na kujali mazingira huku ikizingatia usawa wa kijinsia na haki.

Mwenyekiti wa Bodi ya CRDB Bank Burundi, Hosea Kashimba, alieleza kuwa marathon hiyo ni sehemu ya mkakati wa benki kusaidia juhudi za serikali katika kuimarisha ustawi Burundi.

Aliongeza kuwa tangu benki hiyo ilipoanzisha shughuli zake Burundi miaka 12 iliyopita, imekuwa ikilenga kuboresha ustawi wa kiuchumi na kijamii wa wananchi.

"Tumefanikiwa kuboresha maisha ya mamilioni ya Warundi na tunaendelea kutekeleza dhamira yetu kupitia mbio hizi," alisema Kashimba.

# GUEDE AFUNGUA AKAUNTI YA MABAO SINGIDA BS

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa Yanga, Joseph Guede, amefungua akaunti ya mabao katika timu yake mpya ya Singida Black Stars baada ya kufunga bao pekee lililoipa ushindi wa 1-0 timu yake dhidi ya Aigle Noir ya Burundi juzi.

Guede raia wa Ivory Coast, alisajiliwa na Yanga kipindi cha dirisha dogo la usajili, lakini aliachwa mwishoni mwa msimu huu na sasa amejiunga na timu hiyo.

Ilikuwa ni mechi ya tamasha ambapo timu hiyo ilikuwa ikitambulisha wachezaji wao wapya, pamoja na burudani mbalimbali na hatimaye kukamilishwa na ushindi huo.

Kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Timu ya Mashujaa FC nayo ilikamilisha tamasha lake la utambulisho wa wachezaji kwa ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Inter Star ya Burundi.

Mabao ya ushindi yaliwekwa wavuni na Mundir Vual, Nyeyezi Juma, Ismail Mgunda na Abdulnassir Gamal.

Timu ya Pamba Jiji nayo juzi, ilikamilisha tamasha lake la Pamba Day kwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Vital'O ya Burundi, mechi ikichezwa Uwanja wa CCM Kirumba, Mwanza. Bao la Pamba liliwekwa wavuni na mchezaji mpya aliyesajiliwa kutoka Tabora United, Erick Okutu.

Wakati Singida Big Stars na Mashujaa FC zikipata ushindi kwenye matamasha yao, huku Pamba ikiambulia sare, Timu ya Fountain Gate ilikiona cha moto, ilipodunguliwa bao 1-0 dhidi ya Gor Mahia ya Kenya, katika mchezo wa tamasha lao uliochezwa Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, Babati mkoani Manyara.

Bao pekee katika mchezo huo lilifungwa na Musa Sheriff, akipokea pasi kutoka kwa Alpha Onyango.

**HONGERA...**



Waziri wa Uhusiano wa Afrika Mashariki, Vijana, Michezo na Utamaduni wa Burundi, Gervais Abayeho (kushoto), akimpongeza Mwenyekiti wa CRDB Bank Foundation, Martin Warioba, baada ya kumaliza mbio za kilomita tano kwenye CRDB Bank Marathon Burundi iliyofanyika jana jijini Bujumbura, ambapo Faranga za Burundi milioni 120, zimekusanywa kwa ajili ya kusaidia waathirika wa mafuriko ya Ziwa Tanganyika. **MPIGAPICHA WETU**

# Mpole aibukia Pamba Jiji FC

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa zamani wa Geita Gold, George Mpole, ametangazwa kuwa mchezaji mpya wa Timu ya Pamba Jiji FC kuelekea msimu ujao wa mashindano.

Mchezaji huyo ametambulishwa juzi kwenye Kilele cha Tamasha la Pamba Day lililofanyika Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza na kuhitimishwa kwa mchezo wa kirafiki kati ya timu hiyo na Vital'O ya Burundi ulioisha kwa sare ya bao 1-1, yaliyofungwa na Erick Okutu dakika ya 55 kwa upande wa Pamba na Hakizimana Ramadhani kusawazisha dakika ya 79.

Pamba Jiji, imemsajili mchezaji huyo akitokea FC St Eloi Lupopo ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo.

Straika huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, aliibuka kuwa mfungaji bora wa Ligi Kuu msimu wa 2021/22, akiwa na mabao 17 ya kufunga, akimpiku straika raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo aliyekuwa akichezea Yanga na sasa Pyramids ya Misri, Fiston Mayele, ambaye alimaliza ligi akiwa na mabao 16.

Baada ya ligi hiyo kumalizika klabu kubwa za Simba na Yanga zilionesha nia ya kutaka kumsajili, lakini ikashindikana na kutimkia DR Congo.

Mbali na kucheza mpira nje ya nchi kwenye klabu hiyo ya DR Congo, straika huyo alianza wasifu wake kisoka kwenye Klabu ya Real Nakonde ya Zambia, 2017, kabla ya kusajiliwa na Mbeya City mwaka huo huo, lakini 2019 alitimkia Geita Gold ambako ndiko alijipatia sifa kubwa kutokana na upachikaji mabao, kabla ya kutimkia tena nje ya nchi na sasa amerejea tena kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

## Prisons kamili kuivaa Pamba

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Tanzania Prisons umesema upo tayari kucheza na timu yoyote ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2024/25 utakaoanza Ijumaa wiki.

Prisons itaanzia ugenini dhidi ya wenyeji Pamba Jiji FC, ambayo imepanda daraja msimu uliopita, katika mchezo utakaopigwa kwenye Dimba la CCM Kirumba jijini Mwanza.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Tanzania Prisons, Chacha Waisaka, alisema wamejipanga vizuri tayari kwa ligi hiyo na kwamba wachezaji wao wana ari na morali ya juu kuelekea mechi hiyo ya ufunguzi.

Alisema ratiba wameiona, hivyo watacheza mchezo wa kwanza na pamba wakiwa ugenini na bahati nzuri ni mechi ya kwanza ya ligi hivyo msimu huu, hivyo hawataki kuanza kwa kupoteza.

„Sisi tupo tayari kucheza na timu yoyote ile, si Pamba tu, tumejipanga kwa ajili ya timu zote kwenye Ligi Kuu," alisema Waisaka.

## JKT Tanzania yaipania Azam

**Na Shufaa Lyimo**

KLABU ya JKT Tanzania imesema kikosi chao kinaendelea kujiwinda kwa ajili ya kukutana na Azam FC Agosti 18, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa klabu hiyo, Masau Bwire, alisema kila mchezaji ana morali ya juu kuelekea kwenye mchezo huo.

„Kikosi chetu kinaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kukutana na Azam FC, tunataka kuanza kwa ushindi msimu huu," alisema Masau Bwire.

Alisema kutokana na mazoezi ya muda mrefu waliyoyafanya anaamini wachezaji watatumia vema maelekezo waliyopewa na mwalimu wao kuhakikisha wanapata matokeo.

Aidha, aliweka wazi kuwa msimu huu utakuwa na upinzani mkubwa kutokana na maandalizi yaliyofanywa na kila timu.

Bwire alisema wachezaji ambao wamewasajili msimu huu wataongeza ushindani kwenye kikosi chao, hivyo kuomba mashabiki wao waendelee kuwapa ushirikiano kama walivyofanya msimu uliopita na kwamba malengo yao ni kushika nafasi ya juu kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**FELIX AWINDWA VILLA**
KOCHA wa Aston Villa, Unai Emery, anataka kumsajili mshambuliaji wa Ureno, Joao Felix mwenye umri wa miaka 24, ambaye ana nia ya kuondoka Atletico Madrid. ***(BirminghamLive),***

**GORDON ATAKIWA LIVER**
LIVERPOOL inaendelea kumtaka mshambuliaji wa England na Newcastle United, Anthony Gordon. Mpango wa kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, uliporomoka Juni na huenda bei ya Gordon ikapanda. ***(Liverpool Echo)***

**ACHEAMPONG ANYATIWA**
REAL Madrid na Paris St-Germain, zinamtazama mlinzi wa Chelsea, Josh Acheampong mwenye umri wa miaka 18, kama chaguo linalowezekana la beki wa kulia. Mwingereza huyo ni mhitimu wa akademi ya Chelsea. ***(Independent)***

**ZOUMA HUYOOO SHABAB**
MLINZI wa West Ham, Kurt Zouma, anatarajiwa kufanyiwa uchunguzi wa kimatibabu na Shabab Al Ahli baada ya kuafikia makubaliano na Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 29. ***(Sky Sports)***

**BUONANOTTE KWA MIKOPO**
LEICESTER City inakaribia kumnasa kiungo wa kati wa Argentina na Brighton mwenye umri wa miaka 19, Facundo Buonanotte kwa mkopo. ***(Mail)***

**ZUBIMENDI AOMBWA KUBAKI**
REAL Sociedad inajaribu kumshawishi mchezaji anayelengwa na Liverpool, Martin Zubimendi, kukataa kuhamia Anfield. Kiungo huyo wa kati wa Hispania ana kipengele cha kuruhusiwa kuondoka kwa pauni milioni 51. ***(Times)***

**NKETIAH ATAKIWA MARSEILLE**
KLABU ya Marseille ina nia ya kumnunua mshambuliaji wa England na Arsenal, Eddie Nketiah, 25. ***(Sky Sports)***

**LIVER YAKATAA KIBAO**
LIVERPOOL imekataa ofa nyingi kwa mlinzi wa Uholanzi, Sepp van den Berg mwenye umri wa miaka 22. Hoffenheim, Stuttgart, Wolfsburg, Mainz, Borussia Monchengladbach na Bayer Leverkusen zote zinavutiwa naye. ***(Sky Germany)***

**CAJUSTE KUTUA BRENTFORD**
KLABU ya Brentford imekubali mkataba wa mkopo, na kipengele cha kumnunua ambacho kinaweza kuwa cha lazima na cha thamani ya karibu pauni milioni 10 ili kumsaijili kiungo wa kati wa Sweden Jens Cajuste mwenye umri wa miaka 24, kutoka Napoli. ***(Fabrizio Romano)***

**GALLAGHER NA CHELSEA**
MKURUGENZI wa Michezo wa Klabu ya Valencia, Miguel Angel Corona, amesema Atletico Madrid ilijaribu kufuta uhamisho wa kiungo wa kati wa Chelsea na England, Conor Gallagher mwenye umri wa miaka 24 ili kutanguliza mpango wa kiungo wa kati wa klabu yake ya Javi Guerra, 21. ***(Athletic)***

**JAMES NA BIRMINGHAM**
KLABU ya Birmingham City imekubali mkataba na Rennes kuhusu uhamisho wa kiungo wa kati wa Wales, Jordan James, 20. ***(Independent)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: MAN CITY HAIJAWA FITI KWA EPL

**Siwezi kujibu ikiwa tuko tayari, tungeweza kupoteza leo (juzi) ndiyo maana inabidi tusubiri...**

**LONDON, England**

PEP Guardiola amesema hajui kama Manchester City itakuwa tayari kwa ajili ya kuanza kwa msimu mpya wa Ligi Kuu England licha ya kushinda Ngao ya Jamii dhidi ya Manchester United juzi.

City ilishinda kwa penalti baada ya sare ya bao 1-1 kwenye Uwanja wa Wembley Jumamosi.

Kikosi cha Guardiola kitaanza kutetea taji lao dhidi ya Chelsea kwenye Uwanja wa Stamford Bridge wikendi ijayo, lakini amesema hakujifunza mengi kutokana na ushindi dhidi ya United.

"Siwezi kujibu ikiwa tuko tayari," alisema kocha huyo wa City.

"Tungeweza kupoteza leo (juzi), tulikaribia kupoteza zikiwa zimesalia dakika ndiyo maana inabidi usubiri. Nimeona mambo mengi ninayopenda. Dakika 35 za kwanza zilikuwa bora zaidi, zisizotarajiwa kwa muda ambao tuko pamoja.

"Tuko mbali na ubora wetu. Ni kawaida, lakini ni bora tukianza na kombe moja tuliloshinda.

„Ni nzuri zaidi, lakini ukweli hakuna kilichobadilika kwa ukweli kwamba tulishinda."

City walikuwa mbali na kupoteza hadi mchezaji wa akiba Bernardo Silva alipofunga bao la kusawazisha dakika za lala salama kwa mpira wa karibu wa kichwa na kusababisha mchezo kwenda hatua ya changamoto ya mikwaju ya penalti.

"Tunataka zaidi," Guardiola alisema. "Matendo katika nafasi ya tatu ya mwisho anapaswa kufanya mara kwa mara zaidi. Wakati mwingine ana nafasi ya kuchukua mpira na kwenda na anafanya kitu kidogo, lakini ana kitu cha kipekee. Kutoka kwa kusimama, hatua za kwanza za kulia na kushoto ni za kwanza."

# BARCA YAWEKA TAREHE YA MWISHO KWA WILLIAMS

**BARCELONA,** HISPANIA

BARCELONA inataka kueleweka kuhusu mustakabali wa Nico Williams kabla ya kumenyana na timu yake ya sasa ya Athletic Club Agosti 24, mwaka huu, ripoti imedai.

Williams amekuwa akihusishwa na Barca kwa miezi kadhaa nia yao ya kumnunua winga huyo iliongezeka kutokana na kiwango cha juu kwenye Euro 2024 akiwa na Hispania.

90min ilifichua mnamo Julai kwamba mpango wa awali wa Barcelona ulikuwa kumaliza usajili wa Williams kabla ya kusonga mbele kwa kutaka kumnunua Olmo.

Hata hivyo, mazungumzo kuhusu fowadi huyo wa Athletic yalishindwa kusonga mbele na wakaishia kuendelea na mpango wa kumsajili Olmo kutoka RB Leipzig badala yake.

Barcelona bado wanavutiwa na Williams licha ya kuwa hawakuwahi kufanya mazungumzo ya kutaka kumnunua.

Lakini Mundo Deportivo imeripoti kuwa klabu hiyo imejiwekea muda wa kumpeka Katalunya.


Ikiwa Williams bado ni mchezaji wa Athletic wakati watakapozuru Montjuic mnamo Agosti 24, basi Barcelona haitafanya majaribio yoyote zaidi ya kumsajili lkatika dirisha hili.

Iwapo Barca watakosa winga mpya baada ya mechi hiyo, wataanza kutafuta malengo mbadala kabla ya tarehe ya mwisho ya usajili ya Agosti 30, mwaka huu.

Ingawa Barcelona wameingia kwenye matatizo ya kifedha katika miaka ya hivi karibuni, klabu hiyo inaamini iko katika nafasi nzuri ya kuamsha kipengele cha Williams kuruhusiwa cha euro milioni 60.

Winga huyo tayari anafahamu mishahara inayotolewa na Barca, lakini hajaeleza iwapo atakubali ombi lao.

Matumaini ya rais wa Klabu, Joan Laporta, ni kumwongeza Williams kwenye mstari wa mbele wa nyota mwenza wa Euro 2024 Lamine Yamal ili kuwapa changamoto Real Madrid kwenye La Liga.



## Osimhen aomba kuondoka Napoli

**NAPLES, Italia**



MKURUGENZI wa Michezo wa Napoli, Giovanni Manna, amethibitisha kuwa mshambuliaji wao, Victor Osimhen, ameomba kuondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto.

Chelsea inamwania Osimhen kwa muda mrefu na inaeleweka kuwa 'The Blues' bado wanataka kumnunua nyota huyo wa Kimataifa wa Nigeria, licha ya kukaribia kukamilisha dili la pauni milioni 35 kumsajili Samu Omorodion kutoka Atletico Madrid.

Paris Saint-Germain pia wamekubaliana maslahi binafsi na Osimhen, lakini wamekataa kutimiza matakwa ya Napoli ya zaidi ya pauni milioni 100 kwa mshambuliaji huyo, ambaye aliachwa nje ya kikosi kwa mechi ya kwanza ya mashindano ya timu yake msimu huu, Jumamosi.

Alipoulizwa kueleza kutokuwapo kwa Osimhen, Manna alikiri: "Victor ni mchezaji ambaye anataka kuondoka. Ameomba kuondoka.

"Mwaka jana tayari kulikuwa na hali hii, tumetulia kwa sababu tuna wachezaji kikosini wa kuchukua nafasi yake, Osimhen ni mchezaji mwenye nguvu, lakini tunataka kutoa uadilifu kwenye kundi na tunapendelea zaidi kulinda kuundwa kwa kundi la timu. Kisha tutaona kitakachotokea katika siku 20 zijazo."

Chelsea wanasita kufika bei inayotakiwa na Napoli na wanatumai kumsajili Osimhen kwa mkataba wa mkopo wa awali, ingawa wawakilishi wa mshambuliaji huyo kwa sasa hawakubaliani na wazo la uhamisho wowote ambao haujumuishi hakikisho la kuondoka kwa kudumu kutoka Napoli.

Kufanya kazi kwa faida ya 'The Blues' ni nia ya Kocha wa Napoli, Antonio Conte, kuchukua nafasi ya Osimhen na kumweka Romelu Lukaku, ambaye anapatikana kwa ada ya pauni milioni 37.

## Sterling amtetea kocha Maresca

**LONDON,** ENGLAND

WINGA wa Chelsea, Raheem Sterling, amemkingia kifua kocha mpya, Enzo Maresca kwa ziara yao ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani.

'The Blues' walishinda mchezo mmoja tu kati ya mitano, wakiishinda Club America, lakini wakaangukia kwenye vichapo dhidi ya Celtic, Manchester City na Real Madrid, huku pia wakitoka sare na Wrexham.

Wakati wa ziara hiyo, Chelsea ilikosolewa vikali.

Maresca aliajiriwa kutekeleza mtindo wa soka unaotegemea umiliki, kutokana na kipindi cha msimu mmoja cha Mauricio Pochettino kulingana na shinikizo na mabadiliko ya haraka.

Akizungumza na BBC Sport, Sterling alisema anaamini kuwa Chelsea ina mwelekeo sahihi na anamuunga mkono Maresca, ambaye aliwahi kufanya naye kazi hapo awali kule Man City.

"Anaweza kupata bora zaidi kutoka kwangu, bora kutoka kwa timu," alisema Sterling. "Ameingia na kugonga mamlaka yake, jinsi anavyotaka kucheza.

"Ndio, baadhi ya matokeo hayajapendeza, lakini kwa mpira, habari sahihi inapitishwa. Unaweza kuona mifumo inakuja.

"Ni siku za mapema kwa hivyo unaweza kuona tunakotarajia kwenda. Ni mchakato wa kujifunza kwa kikundi kizima na tunashika haraka sana.

"Ligi Kuu inakuja hivi karibuni kwa hiyo nadhani kuna nyakati nzuri mbeleni."

Mechi ya kwanza ya ushindani ya Maresca akiwa kocha wa The Blues itawakutanisha City na rafiki yake wa zamani Pep Guardiola huko Stamford Bridge.

Siku nne baadaye, Chelsea wataanza safari yao ya Ligi ya Uefa Conference wakiwa na mchezo wa nyumbani wa raundi ya mtoano dhidi ya Braga au Servette.



# KAGERA SUGAR YAACHANA NA MINZIRO, YAMTANGAZA NKATA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Kagera Sugar imeachana na Kocha Fred Felix Minziro baada ya kumaliza mkataba wake wa mwaka mmoja, ambapo sasa itakuwa chini ya Paul Nkata, mchezaji wa zamani wa Timu ya Taifa ya Uganda, The Cranes.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Thabit Kandoro, jana alisema wamemchukua kocha huyo baada ya kufanya upembuzi yakinifu na wanaamini ni mwalimu sahihi kwenye kikosi chao.

„Ana falsafa ya kuuchezea mpira na sisi ndiyo falsafa yetu, hivyo tunaendana naye na tulikaa tukamwambia pamoja na mambo yote, lakini sisi tunataka kufanya vizuri. Tumempa malengo kuwa tunataka tuwe katika nafasi zile za juu zinazoziwezesha timu kucheza mechi za kimataifa, umri wetu sasa katika Ligi Kuu umefikia kucheza mechi za Ligi ya Mabingwa pamoja na Kombe la Shirikisho," alisema Kandoro.

Akizungumza baada ya kutangazwa, kocha huyo alisema amekubali kuja nchini kuifundisha timu hiyo kwa sababu inajulikana, hivyo kama akifanya vizuri na yeye pia atapata fursa ya kujitangaza hapa nchini na hata nje.

„Nina imani tukishirikiana tunaweza kufanya vizuri na kila mmoja atafikia malengo aliyojiwekea," alisema kocha huyo.

Kuondoka kwa Minziro kumeendeleza rekodi yake ya kuhamahama klabu mbalimbali za Ligi ya Champioship na Ligi Kuu.

Kabla ya kujiunga na Kagera Sugar, alikuwa Klabu ya Prisons, ambako nako alitua akitokea Geita Gold.

Minziro pia aliingia kwenye kikosi hicho kuchukua nafasi iliyoachwa wazi na Mecky Mexime, ambaye alikuwa ametimkia Ihefu, iliyobadilishwa jina baadaye na kuitwa Singida Big Stars, ambapo nako aliondoka baada ya ujio wa Patrick Aussems, na sasa ni Kocha Mkuu na Dodoma Jiji akienda kuchukua mikoba ya Francis Baraza.

MAZOEZI...



Vijana wa Kituo cha Michezo cha Jakaya Kikwete, wakiwania mpira katika Uwanja wa kituo hicho wakati wakifanya mazoezi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# KenGold yawanasa Ugando, Sangija

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya GenGold imeendelea kufanya usajili ili kukiimarisha kikosi hicho kitakachocheza kwa mara ya kwanza Ligi Kuu Tanzania Bara, kwa kutangaza wachezaji, Hija Ugando, Gerge Sangija na Helbert Lukindo kujiunga nao rasmi kwa msimu ujao.

Taarifa iliyotolewa na klabu hiyo imeeleza lengo la usajili huyo ni kuwapata baadhi ya wachezaji ambao wana uzoefu na Ligi Kuu Tanzania Bara.

Sangija ambaye ni kiungo wa kukaba, alianza kuwika akiwa na Mbao FC, baadaye akasajiliwa na KMC, akatimkia Mbeya City na amesajiliwa na KenGold akiwa anatokea Geita Gold.

Lukindo ambaye ni straika, amesajiliwa kutoka Mbeya City, ambapo mbali na timu hiyo amezichezea Klabu za Mbao FC, Ndanda na Mgambo JKT.

Kwa upande wa Ugando ambaye naye ni straika, amesajiliwa kutoka Coastal Union, wasifu wake kisoka ukianzia kwenye kikosi cha pili cha Simba na kupandishwa timu ya wakubwa kuanzia mwaka 2015 na kucheza hadi 2017 alipohamia Coasta Union.

Usajili wa wachezaji hao unaifanya klabu hiyo ifikishe wachezaji watano ambao imewasajili kwa ajili ya msimu ujao wa mashindano.

Tayari imeshatangaza kumsajili mdogo wa winga wa Kimataifa wa Tanzania, Simon Msuva, James Msuva, akitokea KMC, lakini ikipata saini ya straika hatari wa TMA Stars, Ramadhan Chobwedo, ambaye alikuwa mmoja wa waliofunga mabao mengi kwenye Ligi ya Championship msimu uliomalizika.

KenGold iilishinda vita ya kumwania straika huyo aliyekuwa akitakiwa kwa udi na uvumba na Prisons.

„Nimefurahi sana kwa kusajiliwa na KenGold, nipo hapa kuitetea nembo ya klabu hii, na ninawaahidi mashabiki wa timu kuwa tutapambana sana, japo ni wageni kwenye ligi, lakini lengo letu ikiwezekana ni kuchukua moja kati ya nafasi nne za juu, na ikishindikana kabisa basi tubaki kwenye ligi tukiwa kwenye nafasi nzuri," alisema Chobwedo.

## Simba wawatuliza mashabiki

INATOKA UK. 24

kuzinduka dakika 20 za mwisho.

Mukwala alikosa bao la wazi dakika ya 21, alipomegewa pasi na Jean Charles Ahoua, lakini shuti lake lilitoka nje kidogo ya lango.

Nusura Coastal wasawazishe bao dakika ya 32, wakati Jackson Shiga alipomwacha Mohamed Hussein 'Tshabalala' na kupiga krosi iliyotua kichwani mwa Deusdedit Cosmas, ambaye alipiga kichwa akiwa huru, lakini kiliishia mikononi mwa kipa, Moussa Camara.

Coastal ilifanya shambulizi la kushtukiza langoni mwa Simba. dakika ya 41, lakini shuti la Ramadhani Mwenda lilikwenda nje ya lango. Kipindi cha pili timu zote zilifanya mabadiliko kadhaa, Simba ikionekana kufanya mengi zaidi kwa kuwatoa Debora Fernandes Mavambo, Ahoua, Mukwala, Tshabalala na kuwaingiza, Valentino Mashaka, Valentine Nouma, Kibu Denis na baadaye aliingia Fabrice Ngoma ambaye alitolewa nje kwa kadi pili ya njano iliyoambatana na nyekundu dakika sita kabla ya pambano kumalizika na mwamuzi Ramadhani Kayoko baada ya kumfanyia madhambi Harnest Malonga.

Cosmas hakuwa na bahati kwani dakika ya 55 alipiga kichwa kingine kilichotokana na mkwaju wa faulo, lakini mpira uligonga nguzo ya pembeni kabla haujaokolewa na mabeki wa Simba. Kipa Camara alifanya kazi ya ziada dakika ya 68, alipookoa hatari ambayo ingeweza kuipatia Coastal Union bao.

Ngoma alimpasia Nouma bila kuangalia kama mtu anayekuja, kabla hajamfikia, Bakari Selemani akaupitia na kubaki yeye na kipa, lakini shuti lake liliokolewa kwa mguu na kipa Camara, ambaye pia jana alionyesha uwezo mkubwa akiwa langoni.

Baada ya mechi hiyo, timu zote sasa zinajiandaa na ufunguzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara itakayoanza Ijumaa, Simba ikitarajia kucheza Jumapili ijayo dhidi ya Tabora United, Uwanja wa KMC, Mwenge, Dar es Salaam, huku Coastal ikisubiri hadi Agosti 29, itakapocheza dhidi ya KMC kwenye uwanja huo huo uliopo Mwenge.

## Gamondi ataka rekodi mpya Ligi

INATOKA UK. 24

alisema Gamondi raia wa Argentina.

Wakati kocha huyo akisema hayo, Meneja wa timu hiyo, Walter Harrison, amewataka wanachama na mashabiki kujitokeza kwa wingi msimu huu kwenye viwanja mbalimbali ili kuiunga mkono timu yao.

Meneja huyo alisema kama ambavyo mashabiki wamefanya msimu uliopita na kujichukulia tuzo ya kuingiza mashabiki wengi uwanjani, amewataka kuvunja rekodi ya mashabiki msimu unaoanza Ijumaa wiki hii.

„Timu iko vizuri sana, na inawezekana kuliko hata msimu uliopita, sasa hivi kikosi ni kipana zaidi, yaani kocha anaamua tu nani acheze, hana presha, kwa hiyo mashabiki nao wasiwe na presha, wajitokeze kwa wingi iwe hapa Dar es Salaam au mikoani," alisema.

Michezo
Nipashe Jumatau Agosti 12, 2024

**Guardiola: Man City haijawa fiti kwa EPL**

UKURASA 21



# Simba wawatuliza mashabiki

## ●●●Watamba huu ndio mwanzo, Karabaka naye afurahia rekodi yake, huku...

**KITU HICHO!...**




Kiungo Mshambuliaji wa Simba, Edwin Balua, akijaribu kuachia shuti kali katikati ya safu ya ulinzi ya Coastal Union, kwenye mechi ya kusaka mshindi wa tatu wa Ngao ya Jamii iliyopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jana na kumalizika kwa timu yake kushinda bao 1-0. **MPIGAPICHA WETU**

**Na Adam Fungamwango**

MFUNGAJI wa bao pekee katika mechi ya jana kati ya Simba na Coastal Union, Salehe Karabaka, amewatoa hofu wanachama na mashabiki wa timu hiyo kuwa wasiwe na wasiwasi na timu yao msimu huu kwani itafanya makubwa, akisema ushindi wa bao 1-0 uliopatikana na kushika nafasi ya tatu kwenye Ngao ya Jamii ni mwanzo tu wa shughuli ya msimu mzima.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mchezo huo wa kutafuta nafasi tatu ya michuano ya Ngao ya Jamii jana, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Karabaka alisema ametumwa na wachezaji wenzake kuwaambia wanachama na mashabiki wa timu hiyo hawapaswi kuwa na hofu kwani wapo kwa ajili ya kupambana kuipigania nembo ya Simba.

„Kwa niaba ya wachezaji, ni kwamba tumejiandaa vizuri kwa ligi, Jumapili tunaanza kazi, wajitokeze ndiyo kwanza shughuli inaanza, tunataka kila tunapokwenda kucheza wajitokeze kwa wingi uwanjani ili watushangilie,“ alisema.

Akizungumzia mchezo huo, alisema ulikuwa mgumu kwa sababu wapinzani wao nao walijiandaa na walionekana wamepania kucheza hiyo mechi kuliko hata ilivyokuwa dhidi ya Azam FC.

Karabaka pia alisema amefurahi kuweka rekodi ya kucheza mechi ya kwanza msimu huu na kufunga bao kama ilivyokuwa kwenye Kombe la Mapinduzi mwaka jana, alipocheza dhidi ya JKU.

„Mwaka jana Kombe la Mapinduzi nilicheza mechi ya kwanza tu baada ya kusajiliwa na Simba, nikafunga bao dhidi ya timu niliyotoka, JKU na leo nimecheza mechi ya kwanza ya msimu nimefunga bao, tena dhidi ya timu ambayo nimeshawahi kuichezea, Coastal Union, hii ni rekodi yangu nzuri sana kama mchezaji,“ alisema Karabaka ambaye alikuwa mwiba kwa mabeki wa timu pinzani jana.

Alifunga bao hilo dakika ya 10 ya mchezo, baada ya kazi kubwa iliyofanywa na wachezaji kadhaa wa Simba.

Mpira ulianzia kwa beki wa kulia Kelvin Kijili, ambaye alipanda nao kwenye wingi ya kulia, akapiga krosi katikati iliyomkuta Joshua Mutale ambaye naye aliipeleka kwenye wingi ya kushoto alikokuwa Steven Mukwala, kisha akaukokota mpira akiwa pembeni kabla ya kupiga krosi iliyomkuta mfungaji akiwa katikati ya wachezaji wanne wa Coastal Union, akawazidi ujanja na kuuweka wavuni.

Timu zote mbili zililazimika kucheza mechi hiyo ya kusaka mshindi wa tatu baada ya kufungwa mechi zilizopita, Alhamisi, Coastal ikibamizwa mabao 5-2 dhidi ya Azam na Simba ikafungwa bao 1-0 dhidi ya Yanga.

Katika mechi ya jana, Simba ilitawala robo tatu ya mchezo huo, huku Coastal ikionekana

INAENDELEA UK. 23

## Gamondi ataka rekodi mpya Ligi Kuu msimu huu

**Na Mwandishi Wetu**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amesema moja ya falsafa anazokuja nazo msimu ujao ni kutoruhusu bao kirahisi kwenye mchezo wowote ambao timu yake itacheza.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, alisema timu yoyote inayotaka kushinda mchezo wa mpira wa miguu ni lazima kwanza ihakikishe ina safu bora ya ulinzi ili kutoruhusu mabao rahisi na ya kizembe, hivyo msimu huu pamoja na ubora wa kikosi chake, lakini atahakikisha hilo halitokei.

Alisema hata kama litatokea, basi iwe ni nadra na sababu inayojitosheleza na si uzembe wa timu au mchezaji mmoja mmoja.

„Moja kati ya vitu ambavyo makocha wengi hawapendi ni kuona timu yake inaruhusu mabao kirahisi na kizembe, na tunakwenda kucheza mechi ngumu za kimataifa, Ligi ya Mabingwa Afrika, huko michezo ni migumu na watu wanatumia sana makosa madogo madogo kukuadhibu, hivyo tunaanza kulifanyia kazi kwenye Ligi Kuu,“ alisema.

Hata hivyo, alisema pamoja na hayo yote, lakini hatobadilika kwenye falsafa yake ya kuchezea mpira na kushambulia, badala yake atawataka wachezaji wake kuwa makini na kushirikiana wanapokuwa wanazuia na wala isitafsiriwe kama atakuwa nyuma ya mpira.

„Bado nitacheza vile vile, sitobadilika kiuchezaji, watu wataiona Yanga ile ile ya msimu uliopita na inawezekana ikawa imara zaidi, sisi tunacheza mpira ambao kila mchezaji anashambulia, kila mmoja anakimbia, kila mmoja anajaribu kurudi haraka kukaba tunapopoteza mipira,“

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >